




**Kampuni** Ufaransa kuweka miradi tril. 9.7/- Tanzania

UKURASA 3




**SKRTEL ASTAAFU KUCHEZA SOKA**

UKURASA 22


# Nipashe

Alhamisi Machi 19, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580950

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




# Samia awageuzia kibao wabunge

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### MKURUGENZI WA SHULE MBARONI MADAI KUJERUHI

JESHI la Polisi Mkoa wa Iringa linamshikilia Mkurugenzi wa Shule ya Sun Academy, Nguvu Chengula (50), kwa tuhuma za kumjeruhi...

UKURASA WA 4

### WANAOPOTOSHA CHANJO YA POLIO SASA KUKIONA

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Waziri Kindamba, amesema serikali mkoani hapa itawachukulia hatua kali watu...

UKURASA WA 5

### MBARONI KWA TUHUMA ZA MAUAJI WANAWAKE WATATU

JESHI la Polisi Mkoa wa Katavi, linamshikilia Richard Michael (25), mkazi wa mtaa wa Shanwe, Manispaa ya Mpanda kwa tuhuma za...

## ZAECA yachunguza kampuni ukwepaji kodi wa mamilioni

UKURASA 3



Aina ya gari linalodaiwa kuingizwa na kampuni moja ya Zanzibar bila kulipiwa kodi. **PICHA: MTANDAO**

# Mahakama yatoa neno mgogoro KKKT Konde

UKURASA 2

**MICHEZO** **DJUMA 'OUT' YANGA VS MBEYA KWANZA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya CRDB, Dk Ally Laay (kushoto), akionyesha kitabu cha ripoti ya mwaka 2021 ya benki hiyo, kwa waandishi wa habari jijini Arusha jana, wakati akitoa wito wa kuwakaribisha wanahisa wa CRDB katika Mkutano Mkuu wa 27 wa Wanahisa unaotarajiwa kufanyika Jumamosi Mei 21 mwaka huu katika Ukumbi wa AICC na kupitia mtandao. Katikati ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Abdulmajid Nsekela na Mkurugenzi wa Mawasiliano, Tully Mwambapa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia awageuzia kibao wabunge

**Na Richard Makore**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka wabunge wahimize wafanyabiashara nchini kulipa kodi ili kuongeza mapato yanayokwenda mfuko mkuu wa serikali badala ya kudai maendeleo katika maeneo yao bila kuwajibika.

Alitoa kauli hiyo jana mkoani Tabora wakati wa uzinduzi wa barabara ya Tabora-Mpanda yenye urefu wa kilomita 342.9 iliyogharimu Sh. bilioni 473.95.

Alisema wabunge wanayo nafasi kubwa kuhakikisha wanasimamia na kuhimiza ulipaji wa kodi katika maeneo yao ili kusaidia wananchi kupata maendeleo.

Rais alisema serikali haina muujiza wa kupata mapato bila kukusanya kodi kutoka kwa wananchi, wakiwamo wafanyabiashara, na kwamba wabunge wanayo nafasi ya kusaidia jambo hilo.

"Serikali haina muujiza katika jambo hili, ni lazima wabunge wahakikishe wanahimiza ukusanyaji wa mapato yanayokwenda mfuko mkuu wa serikali ili fedha hizo zisaidie kuwaletea wananchi maendeleo," alisema.

Rais Samia alisema wabunge wanaposimama na kudai maendeleo katika majimbo yao bila kuhimiza ukusanyaji wa mapato, inakuwa kazi ngumu.

Alitaka wafanyabiashara wote, wakiwamo wenye maduka madogo, kufikiwa na kulipa kodi ya serikali.

Kuhusu ujenzi wa miundombinu ya barabara nchini, Rais Samia alisema serikali itaendelea kufanya hivyo huku akiwataka wakuu wa mikoa kuvutia wawekezaji katika maeneo yao.

Aliishukuru Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) kwa kuendelea kuiamini Tanzania na kuipatia mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya kujenga miundombinu ya barabara.

Alisema mikopo ya namna hiyo inasaidia kujenga barabara na kufungua mikoa na fursa za biashara za ndani na nje ya nchi.

"Benki ya Maendeleo ya Afrika inastahili kuitwa hivyo. Kwa sasa inafanya kazi kubwa katika kuhakikisha tunapata miundombinu ya barabara," alipongeza.

**UHUJUMU UCHUMI**

Rais Samia pia alionyesha kukerwa na baadhi ya watu walioanza kung'oa nguzo za taa katika barabara hiyo na kuonya kuwa huo ni uhujumu uchumi.

Aliwataka wananchi wote kuendelea kutunza miundombinu ya barabara badala ya kuihujumu ili iwanufaishe wananchi wote badala ya mtu mmoja mmoja.

Kuhusu ufugaji wa ng'ombe, Rais Samia aliwataka wananchi kupunguza idadi ya mifugo na kufuga kisasa, akifafanua kwamba kuwa na ng'ombe wengi hakumnufaishi mfugaji bali kunachangia kuharibu mazingira ikiwamo uoto wa asili na hata kusababisha ukame.

"Siyo fahari kuwa na ng'ombe wengi ambao hawaleti maendeleo kwa mfugaji, ni afadhali kuwa na mifugo michache ambayo inamnufaisha mtu," Rais Samia alisema.

Alitoa mfano kuwa mifugo mingi inasababisha kuwapo ukame huku akiagiza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kukaa pamoja kuangalia namna ya kupanga matumizi bora ya ardhi.

**UHABA WA MBOLEA**

Rais Samia pia alisema kiwanda cha mbolea kinachojengwa mkoani Dodoma kitasaidia kupunguza tatizo la upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa wakulima.

Alisema wakati wa ugonjwa wa UVIKO-19, viwanda vingi duniani vilifungwa na kwamba baadhi vilizalisha mbolea chini ya kiwango na hivyo nchi nyingi zilikataa na kuirudisha ilikozalishwa.

Alisema hatua hiyo ilisababisha kukosekana kwa mbolea katika maeneo mengi nchini na hivyo kusababisha wakulima kupata shida.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema barabara hiyo iliyozinduliwa itasaidia kuimarisha biashara katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Rukwa, Katavi na nchi jirani.

Alisema Sh. bilioni 115.89 zimebaki katika ujenzi huo na kwamba zitasaidia kujenga barabara nyingine ambayo itaunganisha mikoa hiyo ya Kanda ya Magharibi.

Meneja wa AFDB, Dk. Patricia Laverley, alisema wataendelea kuisaidia Tanzania katika kujenga miundombinu ya barabara.

Alisema kabla ya kujengwa kwa barabara hiyo wananchi walikuwa wakipata shida kusafiri kwa kutumia njia hiyo na kwamba walikuwa wanatumia zaidi ya saa nane kutoka Tabora kwenda Katavi, lakini kwa sasa wanatumia saa tatu katika safari hiyo.

# Mahakama yatoa neno mgogoro KKKT Konde

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, imeridhia ombi la kufanyika kwa kikao cha usuluhishi nje ya Mahakama kati ya upande wa aliyekuwa Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Konde, Dk. Edward Mwaikali na Askofu Mteule, Mchungaji Geofrey Mwakihaba.

Dk. Mwaikali ndiye aliwasilisha maombi ya kupinga uamuzi wa kuondolewa madarakani dhidi ya uongozi mpya chini ya Askofu Mteule Mwakihaba ambaye alichaguliwa kwenye mkutano mkuu uliofanyika Machi 22 mwaka huu na kusimamiwa na Mkuu wa Kanisa hilo nchini Askofu Dk. Fredrick Shoo.

Jaji James Karayemaha alitangaza uamuzi huo, jana wakati wa kusikiliza shauri hilo ambalo lilihusisha waumini, viongozi wa Kanisa hilo na mawakili wa pande zote mbili.

Jaji Karayemaha alitoa baraka za kufanyika kwa maridhiano ya pamoja nje ya mahakama na kwamba njia hiyo ni nzuri kwani itawaleta pamoja viongozi wote hao na kujadili namna bora ya kumaliza mgogoro huo, ambao umedumu kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa.

"Nimesikiliza hoja za pande mbili wa wajibu maombi na wapeleka maombi, kimsingi hapa busara inapaswa kutumika ili kupata usuluhishi juu ya mgogoro huu licha ya kuwa kila upande una hoja zake lakini, jambo hili linahusu masuala ya imani na dini hivyo kufanyika kwa maridhiano kutaleta amani ndani ya mioyo ya waumini, viongozi wa dini na jamii kwa ujumla," alisema Jaji Karayemaha.

Alieleza mahakama kuwa miongoni mwa majukumu ya chombo hicho ni kushauri kufanyika maridhiano na usuluhishi kwenye mambo yanayohusu imani za kidini ili kutengeneza amani na utulivu na kuokoa gharama za muenendo wa kesi hiyo.

"Nina imani muda wa wiki moja ambao umetolewa kushughulikia mgogoro huu kwa kufanya vikao vya usuluhishi kati ya pande zote mbili ndani ya Dayosisi hiyo ya Konde, utasaidia kesi hii ambayo ilifunguliwa mahakamani hapo kumalizika mapema ili watu wakaendelee na shughuli za maendeleo aliongeza," alieleza Jaji Karayemaha.

Aidha Jaji Karayemaha alimpongeza Dk. Mwaikali kupeleka mahakamani ombi la kufanyika kwa usuluhishi wa mgogoro huo nje ya mahakama kwa maelezo kuwa njia hiyo ni ya busara na inaonyesha imani na utulivu katika Kanisa hilo.

Alisema shauri la ombi la pingamizi kuondolewa madarakani kwa Dk. Mwaikali limepangwa kusikilizwa tena Mei 31, mwaka huu baada ya kikao cha usuluhishi kukaa.

Awali mahakamani hapo, Wakili upande wa mashtaka, Samson Mbamba aliieleza mahakama kuwa kuna mazungumzo ya usuluhishi kuhusu mgogoro huo yameanza yakihusisha viongozi wa pande zote mbili pamoja na vyombo vya serikali.

Aliiomba mahakama kuwa ni vyema shauri hilo likasimamishwa kwanza mahakamani ili kuruhusu vikao vya maridhiano vifanyike ndio hatua nyingine ziendelee.

Wakili upande wa utetezi, Dk. Daniel Pallangyo alieleza kuridhia kufanyika kwa vikao vya usuluhishi ili kumaliza mgogoro huo licha ya hapo awali kuomba shauri hilo liendelee kwani hakukuwapo taarifa zozote juu ya kuanza kwa usluhishi.

Baada ya mahakama hiyo kutoa ridhaa ya kufanyika Dk. Mwaikali aliwaomba viongozi wa kanisa hilo waumini na watu wengine kudumisha amani na utulivu wakati suala hilo likiendelea kufanyiwa kazi.

Mgogoro huo ulianza kufukuta baada ya kuhamishwa kwa Makao Makuu ya Dayosisi hiyo kutoka Tukuyu wilayani Rungwe kwenda jijini Mbeya na kusababisha pande mbili kuanza kusigana.

## HABARI KITAIFA

# ZAECA yachunguza kampuni ukwepaji kodi mamilioni

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), imesema inafanya uchunguzi wa ukwepaji wa kodi Sh. milioni 308.5 dhidi ya Kampuni ya Turky Mifuko, inayomilikiwa na mfanyabiashara maarufu visiwani humo.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Ahmed Makarani, amesema uchunguzi unafanyika baada ya kampuni hiyo kuingiza gari la kifahari aina ya Benz, Januari mwaka huu kupitia Bandari ya Malindi Zanzibar.

"Tunaendelea na uchunguzi na tutatoa taarifa baada ya siku sita na tumefikia hatua kubwa mpaka sasa kuhusu suala hili," alisema Makarani.

Kwa upande wake, Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Kodi ya Mapato Zanzibar (TRA), Juma Hassan Hassan, alikiri gari hiyo kuingizwa mwezi Januari na kuruhusiwa kutoka baada ya wahusika wa dhamana ya Bima wakiendelea kukamilisha msamaha wa kodi kupitiwa kwa Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar.

Hata hivyo, alisema maombi ya kutaka kusamehewa kodi kupitia kwa waziri yalikataliwa na wahusika kutakiwa kulipa kiasi hicho cha fedha, lakini mpaka sasa bado hawajatekeleza "Hatuwezi kuachia kiwango kikubwa cha fedha kupotea tunaendelea kuwafuatilia kupitia mamlaka nyingine mpaka walipe.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu sakata hilo, Kaimu Meneja Huduma za Jamii Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), Makame Khamis Mohamed, alithibitisha gari hiyo kusajiliwa na kupewa namba Z-1 baada ya kukamilisha gharama za malipo ya Sh. milioni 15, mwezi Januari mwaka huu.

"Tulichowapa ni usajili wa namba ya gari baada ya kukamilisha malipo ya milioni 15, lakini kadi ya gari hatujawapa kwa sababu hatujapata nyaraka za malipo ya kodi kutoka Mamlaka ya Kodi ya Mapato Tanzania (TRA) na kama gari inatembea mitaani wanafanya kinyume na sheria.

Hata hivyo, alisema watawasiliana na mamlaka za kusimamia sheria ili kuhakikisha gari hiyo haitembei barabarani kabla ya kukamilisha malipo ya kodi kwa sababu ni kinyume na sheria ya usajili wa vyombo vya moto ya Zanzibar.

Mmiliki wa Kampuni hiyo, Toufkr Salum Toufky, alisema kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji ya Zanzibar wanapaswa kunufaika na msamaha wa kodi kupitia kwa Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar.

Alisema kwamba Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), tayari imewapa barua ya kupinga maamuzi ya waziri ya kutaka kulipa kiasi hicho cha kodi na tayari wamewasilisha katika mamlaka za kusimamia ukusanyaji wa mapato visiwani hapo.

"Baada ya siku sita tutatoa taarifa kuhusu suala hili, lakini ZIPA wametofautiana na maamuzi ya waziri na tunasubiri utekelezaji wa mamlaka za kukusanya mapato Zanzibar," alisema Toufky.

Sakata la gari hilo limeibua mjadala visiwani Zanzibar wakati serikali ya awamu ya nane ikiendelea na mpango wake wa kupambana na ubadhirifu wa mali za umma na kuimarisha misingi ya utawala bora tangu Rais Hussein Mwinyi, aliposhika wadhifa huo.



Balozi wa Ufaransa hapa nchini, Nabil Hajlaoui (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, wakati alipokutana na wafanyabiashara wa kampuni 40 kutoka nchini humo wanaotaka kuwekeza hapa nchini. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kampuni za Ufaransa kuwekeza miradi ya trilioni 9.7/- Tanzania

**Salome Kitomari na Faustine Shija**

UJUMBE wa wafanyabiashara 40 wa kampuni kubwa za Ufaransa umeingia nchini kwa lengo la kuweka mipango ya kuwekeza zaidi ya dola za Marekani bilioni 4.2 (sawa na Sh. trilioni 9.76) kwa makubaliano ya sekta za umma na binafsi za Ufaransa.

Hayo yalibainishwa jana na ujumbe wa kampuni hizo uliokuwa nchini kwa ziara ya kikazi kuanzia Mei 16 hadi jana uliokutana na viongozi wa serikali, sekta binafsi na wadau wengine kwa ajili ya kuangalia fursa na maeneo ya ushirikiano.

Wakizungumza na waandishi wa habari nyumbani kwa Balozi wa Ufaransa nchini, Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Afrika ya Shirikisho la Waajiri nchini Ufaransa, Gerard Wolf, alisema kundi hilo ni kubwa kusini na mashariki mwa Afrika kutembelea nchini.

Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui, alisema ugeni huo umekuja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kutembelea nchi hiyo Februari mwaka huu na kufanya mazungumzo na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, ambao kwa pamoja walikubaliana kushirikiana kwenye sekta mbalimbali.

Wolf alisema kampuni hizo ziko chini ya umoja wao wa Bpifrance, Business France na MEDEF International, ukiwa na wataalamu katika sekta za usafiri, nishati, majisafi, kilimo, chakula na afya zenye lengo la kukidhi mfumo wa ikolojia ya Tanzania ili kukidhi mahitaji ya soko.

"Ziara ya ujumbe huu imechochewa na nia ya dhati ya kampuni za Ufaransa kwa Tanzania, nchi ambayo kutokana na ukuaji wake wa nguvu na utulivu wa kisiasa, inatoa matarajio makubwa ya maendeleo kwa wataalamu wa Ufaransa," alisema.

"Fursa hizi zinatia matumaini zaidi kwani nchi inajitahidi kurejesha hali ya biashara inayowafaa wawekezaji wa kigeni. Wakati wa mkutano wa viongozi wetu (Samia na Macron), walisisitiza juu ya mageuzi ya biashara bora na kukaribisha kampuni za Kifaransa," alisema.

Kwa mujibu wa Hajlaoui, Ufaransa inashikilia wadhifa wa urais wa Umoja wa Ulaya, hivyo inakusudia kuisaidia Tanzania kuhamasisha vyombo vya ushirikiano wa Ulaya huku akitolea mfano wa mpango wa Global Gateway wa Euro bilioni 300 katika uwekezaji) ili kuipa nchi miundombinu bora na endelevu.

Pia alisema kampuni za Ufaransa nchini zimeongezeka zaidi ya mara tatu kuanzia 12 mwaka 2019 hadi 40 mwaka huu, jambo linalodhihirisha uwapo wa raia wa Ufaransa umepanuka katika biashara ndogo, za kati na kubwa.

Aidha, alisema Ufaransa inatarajia kufadhili awamu ya sita ya ujenzi wa miundombinu ya mwendokasi Dar es Salaam na maeneo mengine nchini ili kuwawezesha Watanzania wa maeneo ya pembezoni kufanya shughuli zao kwa urahisi zaidi.

Kwa mujibu wa Wolf, nchi hiyo iko mbioni kuwa mwekezaji mkuu wa Ulaya nchini kwa kuwa ina nia ya kuongeza ushiriki wake wa moja kwa moja katika miradi ya maendeleo hasa usambazaji na uzalishaji wa nishati kupitia kampuni ya Ufaransa kama vile Total Energie na Maurel & Prom.

Alisema eneo jingine ni usafiri na vifaa kama vile ushirikiano na Airbus na mradi wa kukarabati Terminal II katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) na Bouygues Batiment International.

"Kampuni za Ufaransa zimejipanga pia katika maeneo mengine kama vile usafi wa baharini (mradi wa Bagamoyo), maji na usafi wa mazingira, mawasiliano ya simu yaliyozinduliwa hivi karibuni na Eurelsat ya huduma yake ya mtandao ya kasi ya satelaiti kupitia kampuni tanzu ya Konnect Broadband Tanzania, afya hospitali ya Dodoma na msaada kwa vituo vya saratani nchini," alifafanua.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA U J E N Z I , UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA.

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe 15.05.2022 hadi 29.05.2022 kampuni ya Spedag Interfreight itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Holili kuelekea Moshi, gari hilo lenye namba za usajili:
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - Mita 21, Upana - Mita 4.3, Kimo -Mita 5.3**
3. Njia itakayotumika: Holili hadi Moshi kupitia Soweto, gari litasafiri muda wa mchana tu

**( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**



JCL JOSINA CO. LTD
JOSINA COMPANY LIMITED & AUCTIONEER.

**DALALI WA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA – MWANZA,GEITA,BUKOBA,MUSOMA,**
**DEBT COLLECTIONS & AUCTIONEERING**
***HEAD OFFICE –Buzuruga plaza 2nd Floor Room No. 207 Mwanza***
***P.O BOX 11126 MWANZA, 0713/0789/0768-203040***
**josinacompany@gmail.com,josinacoltd@gmail.com**

216861802

**TANGAZO TANGAZOTANGAZO**

*JOSINA COMPANY LIMITED ITAENDESHA MNADA WA HADHARA WA KUUZA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU WA **LETSHEGO BANK TANZANIA LIMITED** KUANZIA 06/06/2022 NA KUENDELEA MUDA NI KUANZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA*

| NA | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | JINA LA DALALI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MOHAMED AMANI RAMADHAN | NYUMBA PLOT NO.1ABlockAIX Kirumba | KIRUMBA | JOSINA CO LTD |
| 2. | JOHN BHOKE GENTEGAI | KIWANJA PLOT NO.1475 Block 'A'Luchelele | LUCHELELE | JOSINA CO LTD |
| 3. | DOTUNATA L.NYALU (2M INVESTMENT) | NYUMBA PLOT NO.248 BLOCK 'A' KABUHORO | KABUHORO | JOSINA CO.LTD |
| 4. | JOSEPHAT E.MARWA | KIWANJA PLOT NO.218 BLOCK 'X' CAPRIPOINT | CAPRIPOINT MWANZA | JOSINA CO.LTD |
| 5. | OMARY MOHAMED ATHUMAN | NYUMBA MBILI ZIKO KWENYE KIWANJA KIMOJA | NDALA B SHINYANGA | JOSINA CO.LTD |
| 6. | MARTHA P.MALYAWERE | HOUSE PLOT NO.529 BLOCK' H' NYAMANORO | JIRANI NA MATAKO BAR | JOSINA CO.LTD |
| 7. | FADHANA SEIF SENKUNI/WEMA H.GILALA | KIWANJA PLOT NO.57 BLOCK 'I' BUGARIKA | BUGARIKA | JOSINA CO.LTD |
| 8. | ULIMWENGU LUCAS KITUMBU | HOUSE PLOT NO 156 Block 'H' East Nyasaka | KANGAE 'B' | JOSINA CO.LTD |
| 9. | PAUL NGWELLE DOTO | NYUMBA PLOT NO. 109 BLOCK 'A' KITANGIRI | JIWE KUU KITANGIRI | JOSINA CO.LTD |

**MASHARTI YA MNADA;**

1. DHAMANA ZITAUZWA KAMA ZILIVYO, MNUNUZI ATALIPIA 25% YA BEI YA MNADA. 75% ITALIPWA NDANI YA SIKU 14 KUTOKA SIKU YA MNADA. AKISHINDWA KULIPA, MALIPO YA AWALI HAYATARUDISHWA.
2. GHARAMA ZA KUBADILISHA HATI ZA UMILIKI ZITAKUWA JUU YA MNUNUZI.
3. UKAGUZI WA DHAMANA ZINAZOUZWA UTAANZA SIKU MOJA KABLA YA MNADA NA GHARAMA ZA KUMPELEKA MTEJA KWENYE DHAMANA ZITAKUWA JUU YA MTEJA.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:-**
**MKURUGENZI Josina Co. Ltd: 0768 203 040, WHATSAPP NO: 0713 203 040**

# Mkurugenzi wa shule mbaroni madai kujeruhi

**Na Francis Godwin, IRINGA**

JESHI la Polisi Mkoa wa Iringa linamshikilia Mkurugenzi wa Shule ya Sun Academy, Nguvu Chengula (50), kwa tuhuma za kumjeruhi kwa kitako cha bastola mzazi aliyekwenda shuleni huko kuomba kuhamisha mtoto wake kwenda shule nyingine.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi, aliwaambia wanahabari jana kuwa tukio hilo lilitokea majira ya saa sita mchana Mei 16, mwaka huu, katika eneo la Shule ya Sun Academy iliyoko Mawelewele mjini Iringa.

Kamanda Bukumbi alidai Chengula alimjeruhi Alifa Mkwawa, maarufu Wilbert (35), mjasiriamali mkazi wa Isakalilo mjini Iringa kwa kutumia kitako cha bastola yake aina ya Cabin 55 yenye namba za usajili 6472-15100082 anayomiliki kihalali na kumsababishia jeraha sehemu ya kichwani.

"Hatua hiyo ilijitokeza baada ya mlalamikaji kwenda shuleni hapo na mwenza wake Prisca Kimaro (30), mjasiriamali wa Isakalilo, kwa nia ya kuomba uhamisho wa mtoto wao (6) anayesoma darasa la pili shuleni hapo," alidai.

Alisema kuwa chanzo cha mzozo ni mtuhumiwa kugoma kutoa uhamisho wa mwanafunzi ambaye ni mtoto wa mlalamikaji.

Alisema mtuhumiwa amekamatwa pamoja na kielelezi cha bastola ambayo imehifadhiwa kituoni na pindi upelelezi utakapokamilika, atafikishwa mahakamani.



Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Mathew Kundo (katikati), akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania Plc, Sitholizwe Mdlalose (kushoto) na Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano Vodacom, Rosalynn Mworia, wakati akiingia kwenye mdahalo wa 'Internet of Things (IOT)' sambamba na Wiki ya Ubunifu 2022, jijini Dodoma jana, lenye mada ya ubunifu kwa maendeleo endelevu. Vodacom Tanzania ni mdhamini mkuu wa Wiki ya Ubunifu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaopotosha chanjo polio kukiona

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Waziri Kindamba, amesema serikali mkoani humo itawachukulia hatua kali watu wanaopotosha kwamba chanjo ya polio sio iliyokuwa ikitolewa kwenye ratiba ya kawaida.

Kindamba aliyasema hayo jana wakati akizindua zoezi la chanjo awamu ya pili kuanzia Mei 18 hadi 21 katika kituo cha afya Njombe mjini.

"Wapo watu wanaosema hii ni kitu kingine, hapana ni ile ile ambayo huwa watoto wanaipata, tumeamua kuchukua hatua kwa sababu tayari imeshatokea mlipuko katika nchi ya jirani kwa hiyo ni lazima na sisi tujikinge waswahili wanausemi unaosema mwenzio akinyolewa wewe wekeza maji kwa hiyo tumeamua kujilinda na kujikinga mapema," alisema Kindamba.

"Kama mtoto alishapata chanjo mara ya kwanza haijalishi ni lazima pia afanye tena kwa mara ya pili hii, naomba niwahakikishie chanjo hii ni salama na inatolewa bure. Akija mtu akikwambia kuna malipo yoyote huyo ni tapeli sio mkweli," alitahadharisha.

Alisema pia, licha ya kupita nyumba kwa nyumba, wataalamu wa afya wapite katika shule za awali ili kuhakikisha watoto waliopo shuleni wanapata chanjo.

Naye Mganga Mkuu Halmashauri ya Mji Njombe, Isaya Mwasubila, alisema kuwa kama halmashauri wamejipanga kuhakikisha kila kituo cha kutolea huduma wamesambaza chanjo.

Alisema katika awamu ya kwanza walifikisha zaidi ya asilimia 100 na awamu ya pili watavuka zaidi ya malengo waliojiwekea.

"Tunataka kumfikia kila mtoto, nyumba kwa nyumba na katika vituo vyote vya kutolea huduma ili kuhakikisha kila mtoto anafikiwa anapewa matone na anakingwa dhidi ya ugonjwa wa polio," alisema Mwasubila.

## Taasisi yapata dawa ya uhaba wa walimu

**Na Getrude Mbago**

KATIKA kukabiliana na uhaba wa walimu na wingi wa wanafunzi madarasani nchini, Aga Khan Foundation imezindua mfumo rafiki wa kupambana na tatizo hilo kwa kuwafanya walimu kuwa na mbinu bunifu.

Mfumo huo unatekelezwa kupitia mradi wake wa miaka 10 wa Schools 2030 na unaotarajiwa kugharimu Dola 500,000, ukitekelezwa kwenye shule mbalimbali za mikoa ya Dar es Salaam na Lindi.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam katika maonyesho ya mbinu mbalimbali zilizobuniwa na walimu, Ofisa Elimu Msingi Manispaa ya Temeke, Abdul Buheti, alisema mradi huo utatatua shida mbalimbali za elimu nchini, ikiwamo kuwasaidia wanafunzi kuelewa zaidi na kumpa mbinu za ziada mwalimu za kufundishia.

Buheti alisema licha ya serikali kuboresha mazingira ya elimu nchini ikiwamo kugharamia elimu msingi bila malipo bado imebainika katika baadhi ya halmashauri zina wingi wa wanafunzi, hivyo kusababisha shida katika utoaji wa elimu huku akitolea mfano katika baadhi ya shule Manispaa ya Temeke.

Buheti alisema baada ya Aga Khan Foundationa kuja na mradi huo, kumepunguza kero zilizobainika baada ya kuwajengea uwezo walimu na kutatua kero zinazowakabili.

Alisema kupitia mradi huo, walimu hutumia mbinu rahisi kufundisha na kufanya wanafunzi waelewe kwa haraka. Hutumia vifaa kama mbao, karatasi za manila na mbinu nyingine nyingi zinazopatikana katika mazingira yao.

Msimamizi wa mradi huo kitaifa, Shaibu Mandola, alisema mradi huo utajikita zaidi katika kukabiliana na kero zinazowakabili walimu katika ufundishaji.

Alisema walimu wengi kwa sasa wana mbinu bunifu za kufundishia na hiyvo kuhakikisha wanafunzi wote wanajifunza na kuelewa somo hata kama wako wengi darasani.

"Tatizo la msongamano darasani siyo changamoto tena kwa walimu hawa kushindwa kufundisha, kwani mradi umewapa mafunzo na kupata mbinu mbadala na rahisi zinazowafanya kufurahia kazi yao na kuwapenda zaidi wanafunzi," alisema.

# Mbaroni tuhuma mauaji wanawake watatu

**Na Neema Hussein, KATAVI**

JESHI la Polisi Mkoa wa Katavi, linamshikilia Richard Michael (25), mkazi wa mtaa wa Shanwe, Manispaa ya Mpanda kwa tuhuma za mauaji ya wanawake watatu yaliyofanyika mwezi uliopita kwa nyakati tofauti katika mtaa wa Ilembo.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Sylvester Ibrahim, alisema jana akizungumza na waandishi wa habari baada ya matukio hayo polisi walifanya msako na kumkamata Crispin John akiwa na simu ambayo ilipokwa kwa marehemu Zainab Abdala baada ya kuuawa Aprili 2, mwaka huu.

Alisema mtuhumiwa baada ya kuhojiwa, alikili kufanya mauaji ya wanawake hao kisha kuwanyang'anya vitu mbalimbali alivyowakuta navyo kama vile simu, mikoba, pesa kisha miili yao kuitelekeza vichakani na kwenye mashamba ya mahindi.

Alisema mtuhumiwa baada ya kukiri, aliwaongoza viongozi mbalimbali wa mtaa, Jeshi la Polisi na baadhi ya familia za marehemu kuonyesha maeneo yote aliyofanyia ukatili huo.

Baada ya kufika katika eneo mojawapo, alisema walikuta viatu vya marehemu ambavyo vilijulikana na ndugu.

Kamanda Ibrahim alisema mtuhumiwa wakati akiliongoza jeshi hilo kwenda eneo la tukio, alilegeza pingu na kisha kukimbia, hivyo kusababisha askari kupiga risasi mbili hewani kumtaka asimame.

Alisema mtuhumiwa hakufanya hivyo ndipo walimjeruhi kwa risasi maeneo ya mgongoni na wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Katavi, alifariki dunia.

# Mpango aipongeza UN kuanzisha mfumo kuhusu masuala ya kijamii

**Na Maulid Mmbaga**

MAKAMU wa Rais Dk. Philip Mpango ameupongeza Umoja wa Mataifa (UN) kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kuanzisha mfumo utakaoshughulikia masuala ya kijamii ambayo yatasaidia kuleta maendeleo endelevu katika nyanja mbalimbali.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika uzinduzi wa Mfumo wa Ushirikiano wa Maendeleo Endelevu wa Umoja wa Mataifa (UNSDCF), ambao utafanya kazi kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwezi Julai mwaka huu hadi Juni, 2027.

Alisema mfumo huo utasaidia mambo mbalimbali ya nchi ikiwamo kuongeza uzalishaji, mapato, kupata ajira nzuri na bora, ukuaji endelevu na mabadiliko ya ujumla ya ukuaji wa rasilimali ya nchi kwa maslahi ya wananchi kwa ujumla.

"Kama nchi tunaahidi kufanya kazi na nchi zingine ambazo ziko chini ya Umoja wa Mataifa kurudisha amani duniani na kupata uchumi wa dunia na ukuaji taifa," alisema Dk. Mpango.

Kwa upande wake, Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa nchini Tanzania (UN) Zlatan Milisic, alisema mfumo wa umoja huo nchini Tanzania umebaini maeneo manne ya kimkakati, kwa kuongozwa na Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya 2030, ambayo wanalenga kuyashughulikia kupitia mfumo mpya wa ushirikiano.

Alibainisha eneo la kwanza la kimkakati kuwa ni watu, akieleza kuwa katika eneo hilo UN itashirikiana kuimarisha ustawi wa Watanzania, sasa na siku zijazo, pia litalenga viwango vya uzazi miongoni mwa vijana balehe, vifo vya kina mama, VVU, Kifua Kikuu na Malaria, Elimu, Lishe, na Kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Eneo la pili la ni utajiri na kuimarika kiuchumi, akifafanua kuwa mkazo wa UN katika eneo hilo la kipaumbele ni kuongeza uzalishaji, tija na kipato na kusaidia kuongeza kasi ya utengenezaji wa ajira zenye hadhi katika sekta rasmi.

"Hii itafikiwa kupitia kazi yetu ambayo itakazia kipato na tija za wazalishaji wa chakula, mifumo ya chakula, mbinu za kilimo, ujasiriamali, msaada kwa biashara ndogo kabisa, ndogo na za kati na ujumuishi wa kifedha," alisema Milisic. Eneo la tatu ni Sayari, ambalo alisema kuwa litaunga mkono ulinzi wa mazingira, mbinu za maendeleo zilizo endelevu, ambazo zitajumuisha upatikanaji wa nishati na teknolojia rafiki zitakazochochea ukuaji na kuwezesha usimamizi ulio endelevu zaidi wa utajiri wa rasilimali za Tanzania.

Eneo la nne ni mazingira wezeshi katika kujenga ushirika na amani, alisema eneo hilo linakazia katika masuala mapana ya uwakilishi na utawala jumuishi, upatikanaji wa data, uwekaji mipango ya maendeleo na utoaji fedha, upatikanaji wa haki, kudumisha amani, na kupanua uingizwaji wa masuala ya usawa wa kijinsia na haki za binadamu.

Alisisitiza kuwa kuhakikisha wanapambana kukamilisha na kutekeleza mfumo wa UNSDCF, timu ya nchi ya Umoja wa Mataifa itafanya jitihada maalumu.

Alibainisha jitihada hizo ikiwamo kubaini makundi ya watu na maeneo ya kijiografia ambayo yameachwa nyuma zaidi, kupitia ukusanyaji na uchambuzi makini wa data, ikiwamo kutambua maeneo yenye hatari na utafiti wa kiutendaji na kuamua njia bora zaidi za kuweka madaraja ya kujinusuru.

Jitihada ya pili ni kuanzisha ushirika imara zaidi na sekta binafsi na kwa kutumia manufaa ya fursa ilizo nao Umoja wa Mataifa na mamlaka ya kukutanisha pande mbalimbali, kusaidia jitihada zitakazoongeza rasilimali za kugharimikia maendeleo.


**BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **NMB BANK** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne(14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa aliyetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) zilizodhamini mkopo wake kwa MNADA WA HADHARA.Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana zilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAWI |
|---|---|---|---|
| 1. | SPRINT CORPORATE LIMITED/BEATUS GODBET RUGE | Kiwanja kilichopo maeneo ya Kulangwa Manispaa ya **Kinondoni,** Dar es salaam kwa jina la **Beatus Godbet Ruge** | TEGETA |
| 2 | JOYCE GIDIONI KWAYU | Nyumba ya makazi iliyopo Vianzi, Wilaya ya Mkuranga,Pwani. | KARIAKOO |
| 3 | NASSIR FOCUS NDESSI/THERESIA ERICK SHAYO | Nyumba yenye leseni ya makazi na. TMK041580 iliyopo Mianzini Charambe, Manispaa ya Temeke kwa jina la Theresia Erick Shayo | KARIAKOO |
| 4 | YUSUPH MBOETO | Nyumba ya makazi iliyopo mabibo sahara yenye leseni ya makazi KND/MBB/MBO16/114 Manispaa ya ubungo | ILALA |
| 5 | ZAHARA HUSSEIN | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye Kiwanja chenye **Leseni** ya makazi maeneo ya **Mangaya Mbagala TMK/MBGL/MAN11/269A Manispaa** ya **Temeke** | MBAGALA |
| 6 | BAKARI SELEMANI BANYANGA | Nyumba ya makazi yenye Hati ya mauziano iliyopo maeneo ya Mbagala Kilungule | KARIAKOO |
| 7 | BENSON NAHUM KABERE | 1) Nyumba ya makazi yenye kipande cha ardhi na.TMK/MBGL/KZG5/299 yenye leseni no TMK032102 iliyopo kizinga manispaa ya temeke<br>2) Nyumba ya makazi yenye kiwanja no 28&29 kitalu H leseni no.139102 na no.551610 iliyopo chamazi manispaa ya ilala | KARIAKOO |
| 8 | YUSRA ALLY RAMBO | Nyumba ya makazi iliopo kwenye kiwanja kilichopo Mtoni relini. | KARIAKOO |
| 9 | HAJI ISMAIL | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye Kiwanja chenye Hati ya mauziano maeneo ya Ponde Twangoma Manispaa ya Temeke. | ILALA |
| 10 | TANTON IMAGING TECHNOLOGY/KUMBUKA DEUS NTEJA | Nyumba ambayo haijakamilika iliyopo kigogo kati yenye leseni ya makazi KDD/KGG/KST11/82 | ILALA |
| 11 | ERICK AMANI SWAY | i. Nyumba ya makazi yenye kipande cha ardhi na.TMK/CHB/KIM2/53 iliyopo charambe mtaa wa kilungule,manispaa ya Temeke yenye Leseni na.TMK035418 kwa jina la Nuhu Ismail Kaitila<br>ii.. Nyumba ya makazi yenye kipande cha ardhi na.TMK/MBGL/MOR2/410 iliyopo Mbagala mtaa wa Moringe, manispaa ya Temeke yenye Leseni na.TMK041863 kwa jina la Juma Hamisi Kitogo | B/CENTRE. |

**MASHART YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Building, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537**

**Au**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**First National Bank**
**1st Floor FNB House**
**Ohio Street**
**P. O. BOX 72290**
**DAR ES SALAAM**



**BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**NOTISI YA SIKU 14/MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **BANK OF AFRICA (BOA)** tunatoa Notisi ya siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili kwa mdaiwa tajwa hapo chini kwenye jeduari alipe deni analo daiwa na benki hiyo Pamoja na riba.kushindwa kufanya hivyo mali iliyowekwa kama dhamana itauzwa kwa njia ya mnada wa Hadhara kufidia deni hilo.Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo tarehe na muda kama inavyoonyeshwa kwenye jeduari hapo chiniinavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | TAREHE |
|---|---|---|---|
| 1. | MKASI AGRI PRODUCTS SUPPLIES LIMITED / BARAKA NSAJIGWA KYEJO | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA. P 5469 ENEO LA UBUNGO MANISPAA YA UBUNGO· | 04.06.2022, JUMAMOSI SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHART YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Building, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537**

**Au**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**First National Bank**
**1st Floor FNB House**
**Ohio Street**
**P. O. BOX 72290**
**DAR ES SALAAM**



**BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent, Court Broker & Legal Consultant

**NOTICE YA SIKU (14)/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK** tunatoa Notisi ya siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili kwa mdaiwa tajwa hapo chini kwenye jeduari alipe deni analo daiwa na benki hiyo Pamoja na riba.kushindwa kufanya hivyo mali iliyowekwa kama dhamana itauzwa kwa njia ya mnada wa Hadhara kufidia deni hilo.Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo tarehe na muda kama inavyoonyeshwa kwenye jeduari hapo chini.

| NA. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | TAREHE |
|---|---|---|---|
| 1. | BIMAT INVESTMENT LIMITED/EMMANUEL GODWIN GAMBI | Nyumba yenye hati miliki no 114905 L.O No ,395221, kiwanja no.69,kitalu Q Eneo la Kibamba. | 02/06/2022.Kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea. |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**

**AU**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**EQUITY BANK LIMITED**
**HEAD OFFICE, Golden Jubilee Towers, 3rd floor, ohio street**
**P. o Box 110183, Dar es salaam,**
**Tel: + 255 768 985500/ +255 746 888 455**
**Website: www.tz.equitybankgroup.com**

216862002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mamlaka zisikubali walimu kudhalilika

**LIPO** tatizo ambalo kwa sababu zisizojulikana halitafutiwi ufumbuzi. Tatizo hili ni mikopo inayotolewa na taasisi mbalimbali za kifedha kwa walimu.

Mikopo ni kitu ambacho hakiwezi kuepukika kwa mtu yeyote, kwa sababu inamwezesha mhusika kupata uwezo wa kifedha kwa ajili ya kutimiza mahitaji yake. Ili mradi anakopa kwa kufuata taratibu rasmi za kukopeshwa na mkopeshaji.

Kwa mujibu wa sheria na taratibu, lazima mkopaji na mkopeshaji waingie kwanza katika mkataba wa kisheria kabla ya kutolewa mkopo, ikiwamo kiwango cha riba, kiwango cha makato, wadhamini na utaratibu mzima wa kurejesha mkopo. Tatizo tunalolizungumzia hapa linahusu mikopo inayotolewa na baadhi ya taasisi za fedha nchini hususani zisizo tasmi kuwakopesha walimu katika maeneo mbalimbali kisha mikopo hiyo badala ya kuwa ya manufaa kwao huwa ya unyanyasaji, udhalilishaji, mateso na fedheha kwa walimu.

Suala la mikopo hiyo maarufu kwa jina la 'mikopo umiza' limekuwa likiripotiwa katika maeneo mengi na matokeo yake kuwaacha walimu na madeni makubwa ya kubambikiwa, ambayo wanashindwa kuyalipa hata baada ya kumaliza muda wao wa utumishi. Kibaya zaidi ni kwamba taasisi hizo zinawalaghai walimu kuwakopesha haraka bila kupitia utaratibu tulioueleza zikijua kuwa kada hii ya watumishi wa umma ina uhitaji mkubwa wa fedha.

Inaelezwa kuwa baadhi ya taasisi hizo huwanyang'anya kadi za benki walimu walioshindwa kulipa madeni na wakati mwingine kufuatwa madarasani kudaiwa kama ilivyoripotiwa wiki hii katika Manispaa ya Shinyanga mkoani Shinyanga.

Baadhi ya taasisi hizo zimekuwa zikiwafuata walimu katika sehemu zao za kazi kuwadai madeni mbele ya wanafunzi bila kufuata au kuheshimu mikataba waliyoingia wakati wanakopeshana. Hatua hiyo imetajwa kuwa sehemu ya vikwazo vinavyorudisha nyuma maendeleo ya elimu kwa kuwa walimu wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu wakihofia kuvunjiwa heshima mbele ya wanafunzi wao, kufungiwa ndani na kupokwa kadi zao za benki. Hili halihusu mkoa wa Shinyanga pekee, ni maeneo yote ya nchi.

Ushuhuda huu umetolewa na mmoja wa viongozi waandamizi wa Chama cha Walimu (CWT) katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, kwamba


kila mwaka kumekuwa na matukio ya baadhi ya walimu kukamatwa na wakopeshaji wa mikopo na kufungiwa ndani katika ofisi zao wanaposhindwa kulipa mikopo kwa wakati, akisisitiza kuwa jambo hilo lisipotatuliwa wanafunzi wataendelea kukosa masomo na kushindwa kumaliza mihula. Kauli hiyo inadhihirisha kuwa tatizo hili ni kubwa, ambalo linahitaji mamlaka husika kuingilia kati kuwanusuru walimu.

Wengi tunaelewa mazingira yasiyo rafiki ambayo walimu wanafanyia kazi hususan katika maeneo ya vijijini. Kwa mfano, yako matukio ya mwalimu kusafiri umbali mrefu kufuata mishahara mijini ngazi ya wilaya na kukuta haijaingizwa benki na kulazimika kuondoka patupu na wakati mwingine wengine wanakuwa wamekopa hata nauli. Katika mazingira kama haya nia rahisi kuchukua mikopo kutoka taasisi hizi kwa kuwa mikopo kutoka taasisi rasmi huchukua muda mrefu kutokana na kuhitaji taratibu.

Kuna baadhi ya hatua zinazoweza kuchukuliwa kuwaepusha walimu dhidi ya hali hii ikiwamo CWT kushirikiana na halmashauri katika kuwadhamini walimu kuchukua mikopo kutoka taasisi za fedha bila kujali kama ni rasmi au isiyo rasmi. Kuna umuhimu pia walimu kusaidiwa kukopa kwenye benki yao ambayo sasa imeunganishwa kuwa sehemu ya Benki ya Biashara Tanzania (TCB), hivyo kupata mikopo isiyochukua muda mrefu wala vikwazo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Ni aibu vyoo vya umma vya kinamama, asafishapo baba

**INAFAHAMIKA** katika jamii choo ni huduma nyeti, pia kiungo muhimu sana katika maisha ya jamii kokote waliko. Ndio maana kaulimbiu inayohamasisha huduma hiyo inasema 'nyumba ni choo.'

Vivyo hivyo, imekuwa jambo la busara sana wakati wote huduma hiyo inapotolewa katika utaratibu wa sasa kisera, hamasa ya wingi wake ikienea sana kwa mvuto wa utaratibu wa malipo, hata kukawepo waendeshaji binafsi.

Unyeti wake unakuwa maradufu, hasa penye maeneo ya mikusanyiko. Hiyo huendana na huduma ya bafu za umma kuoga kwa malipo, kwa kiasi kikubwa gharama zinafanana kwa sehemu nyingi.

Ni aina ya huduma ambazo uendeshaji wake nyuma ya pazia kuna wasimamizi wa afya hasa kutoka maeneo jirani na mahsusi serikali ya mtaa ambao ni wakali sana kuhakikisha kanuni za afya usafi wa vyoo hivyo zinatimizwa.

Kilichopo, pindi pakitetereshwa tu mahali hapo, maana yake ni kwamba, panageuka kuwa chanzo kikubwa cha maradhi ya milipuko, hata shida ya kiafya kuwafikia wengi.

Hilo ni eneo mojawapo. Mara zote katika huduma za umma na hasa za faragha, mipaka ya kijinsia ni muhimu sana kuzingatiwa katika ngazi zote za kiimani hadi kimataifa.

Wamiliki na wasimamizi wa vyoo hivyo huajiri watendaji kushughulikia usafi wake, kama wanavyoelekezwa na kanuni za kitaifa, pia miongozo husika. Hapo ndipo kunazaliwa mzizi mpya wa matatizo.

Pia, milango ya kuingia vyooni inatambulishwa kwa picha za kike na kiume, kila mwenye jinsia yake hufuata njia inayomhusu chooni akapate huduma.

> **Wamiliki na wasimamizi wa vyoo hivyo huajiri watendaji kushughulikia usafi wake, kama wanavyoelekezwa na kanuni za kitaifa, pia miongozo husika. Hapo ndipo kunazaliwa mzizi mpya wa matatizo.**

Pia huduma ya choo inaendana na ya bafu, zote zikiwa na gharama zinazowafikia watumiaji ambazo kwa kiasi kikubwa zinafanana.

Katika huduma za vyoo, wapo baadhi ya wamiliki wameajiri wafanyakazi wa kike na kiume kuzihudumia. Niseme, hapo ndiko mahali jicho langu linafunguka kuona pengo.

Katika baadhi ya vyoo, huduma husika hutolewa na wanaume pekee vyooni na bafuni, ninasikia kwingineko kinadada pekee.

Sasa choo cha wanawake kwa nini asiajiriwe mwanamke asimamie usafi na kuwapatia huduma wanawake wenzake?

Yaani ni aibu kwa nyie wenye vyoo kushindwa kuajiri wanawake kufanya usafi katika vyoo kufanywa na mwenye jinsia tofauti.

Kwa ukweli, kuna mambo mengi katika vyoo vya umma ambayo yanatakiwa kwenye usafi wake, ya mwanamke daima afanye mwanamke, mwenyewe na kamwe sio mwanaume.

Mama huyo anapoingia chooni na anakutana na mwanaume akifanya usafi, hapo tayari ameshaanza kudhalilika. Hana hata ile nafasi ya kujiweka vizuri anapotoka chooni, kwa sababu kuna mwanaume hapo njiani.

Mnaotoa ajira mzingatie hayo, choo cha wanawake kisimamiwe na wanawake na choo cha wanaume, kisimamiwe na wanaume.

Hata ikiangaliwa katika shule za msingi, hili limezingatiwa sana. La watoto wa kiume wanafanya wavulana na la mabinti hufanywa na wasichana.

Hilo ndilo linaonekana katika huduma nyinginezo za umma, mahsusi niko katika hospitali, huwa nawaona wafanyakazi wanaume wanafanya usafi kwa wanaume na wanawake kwa wanawake. Sasa nyie wa vyoo vya kulipia, shida nini?



Mkazi wa Kimara, Ally Kayuni (kushoto), akipokea zawadi ya kitita cha Sh. milioni 10 kwa Meneja Uhusiano wa Benki ya CRDB, Tawi la Palm Beach, Janeth Msuya, baada ya kuibuka mshindi wa bahati nasibu ya Biko, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shahidi adai kufungia vielelezo kabatini

**Na Grace Gurisha**

OFISA Polisi, Idara ya Upelelezi Kitengo cha Kupambana na Kuzia Dawa za Kulevya (ADU), Philimon Mbinda, ameiambia Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuwa ilimlazimu kufungia vielelezo (mirungi) kwenye kabati la chuma kwa sababu mtunza vielelezo hakuwapo.

Mbinda alidai hayo juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Evodia Kyaruzi wakati akitoa ushahidi katika kesi ya dawa za kulevya inayomkabili Fatuma Uroto, Zamiru Juma na Fatuma Sharifu, ambao wanatuhumiwa kukutwa na mabunda 11 ya mirungi.

Shahidi huyo, alidai kwamba baada ya kufika ofisini muda wa saa tano usiku mtunza vielelezo hakuwapo, alichukua vielelezo hivyo na kuvifungia kwenye kabati la chuma na kuondoka na funguo.

Alidai, baada ya kumaliza zoezi hilo aliondoka na kurudi tena ofisini hapo Machi, 2019 saa mbili asubuhi, alienda kufungua kabati hilo na kumkabidhi mtunza vielelezo kwa ajili ya kuvifunga na kuvihifadhi.

Mbinda alidai hayo baada ya kurudishwa mahakamani hapo kwa mara ya pili kutoa ushahidi wake ili kueleza alipovihifadhi vielelezo hivyo, kwa sababu alivikamata na kwenda navyo ofisini.

Awali, Wakili wa Serikali, Tumaini Mafuru alimkumbusha shahidi wake kuwa, Mei 24, 2021 na Septemba 13 alifika mahakamani hapo na kutoa ushahidi, anachotakiwa kuieleza mahakama ni wapi alipoviweka vielelezo baada ya kuvikamata.

Mbinda alidai kuwa, Oktoba 2, 2019 majira ya saa 10 jioni alipigiwa simu na ACP Kabalege akimuelekeza kuwa kapigiwa simu na msiri kuwa huko Magomeni Mapipa, Mtaa wa Tosheka kuna nyumba watu wanafanya biashara ya dawa za kulevya.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Grace Mwanga, Mbinda alidai kuwa alipofika eneo hilo akiwa na askari wengine watatu, PC Ramadhani, PC Gladness na PC Daudi, msiri wao aliwaonesha nyumba hiyo na walipofika waligonga geti na kufunguliwa na kijana mmoja ambaye walimuagiza akamuite mpangaji wa hiyo nyumba.

Alidai kuwa kijana huyo aliingia ndani akatoka na mama mmoja, ambaye alijitambulisha kwake na yeye alijitambulisha kuwa anaitwa Fatuma Uroto, ndiye amepanga kwenye hiyo nyumba na kumueleza walichofuata hapo huku akiongozana naye hadi kwa mjumbe ili kufanya upekuzi wa nyumba.

**Mbinda alidai kuwa, Oktoba 2, 2019 majira ya saa 10 jioni alipigiwa simu na ACP Kabalege akimuelekeza kuwa kapigiwa simu na msiri kuwa huko Magomeni Mapipa, Mtaa wa Tosheka kuna nyumba watu wanafanya biashara ya dawa za kulevya.**

# ACT yaibuka na hoja tisa sekta ya kilimo

**Na Halfani Chusi**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimetaja mambo tisa kinayoamini yanadidimiza ukuaji wa sekta ya kilimo nchini.

Naibu Msemaji Sekta ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi wa chama hicho, Selemani Misago, akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, alitaja mambo hayo na kusisitiza kwamba kama serikali ikiyafanyia kazi, itasaidia kuinua sekta hiyo.

"Kuna maoni kadhaa ambayo serikali inapaswa kuyafanyia kazi ikiwamo kutokupuuza kilimo. Ukuaji wa sekta ya kilimo unaendelea kushuka," alisema.

Misago alisema mambo mengine ya kufanyiwa kazi ni kuhakikisha kilimo kinajibu mahitaji ya ndani; bodi za mazao zimeshindwa kumkomboa mkulima na kuendeleza kilimo; upatikanaji wa mbolea na matumizi ya zana za kisasa.

Pia wingi wa kodi na tozo kwenye mazao; mfumo wa stakabadhi ghalani kuwa kitanzi kwa mkulima; safari ya kufungamanisha kilimo na viwanda bado ni ndefu kutokana na miundombinu mibovu vijijini hususani kwenye sekta ya umwagiliaji; pamoja na kilimo cha kutegemea mvua.

Alisema chama hicho kinaishauri serikali kuwekeza nguvu zaidi kwenye mabonde ya Mto Ruvu, Rufiji, Pangani, Kilombero, Ruvuma, Mbwenkuru, Ruwaha, Kihansi, Mara na Mabonde ya Ziwa Tanganyika na Victoria ili kuboresha mfumo wa umwagiliji kwa mkulima kuliko kutegemea mvua.

"Pamoja na kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC), bado sekta ya umwagiliaji haiwanufaishi wakulima. Tanzania ina mabonde mengi yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, hivyo ni muhimu kwa nchi kuwekeza katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji ili sekta hii iwe na tija kwa wananchi na Taifa lake," alisema.

Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka ujao wa fedha yaliridhiwa na Bunge jana mjini Dodoma, wizara hiyo ikitarajiwa kutumia Sh. bilioni 751, likiwa ni ongezeko la asilimia 155.34 kulinganishwa na mwaka wa fedha 2021/22 uliobakisha siku 43 kufika ukomo.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

**TAARIFA KWA WALIOKUWA WAFANYAKAZI WA MGODI WA DHAHABU WA BULYANHULU**

Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu (OWM-KVAU) kwa nyakati tofauti imekuwa ikipokea malalamiko ya waliokuwa wafanyakazi wa Modi ya Bulyanhulu dhidi ya Mwajiri wao kuhusu kutopimwa afya, kutokupatiwa matibabu na kutokulipwa fidia.

Serikali kupitia Wizara yenye dhamana na masala ya Kazi na Ajira imekuwa ikishughulikia malalamiko hayo kupitia Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA), Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) na Idara ya Kazi.

Kwa mara ya mwisho mnamo mwaka 2021 Wizara yenye dhamana ilipokea, kuchambua na kutolea maamuzi malalamiko 150 ya waliyokuwa wafanyakazi Bulyanhulu. Hata hivyo waliokuwa wafanyakazi wa kampuni hiyo wameendelea kuwasilisha malalamiko katika mamlaka mbalimbali za Serikali.

Ofisi imepokea malalamiko kadhaa ambayo yataanza kuchambuliwa ili kuyatolea maamuzi. Hivyo, ninapenda kuwataarifu wale wote ambao malalamiko yao hayajawahi kuwasilishwa na kutolewa maamuzi na Ofisi ya Waziri Muu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kuwasilisha malalamiko yao ili nayo yafanyiwe kazi kwa pamoja. Malalamiko hayo yawasilishwe mapema iwezekanavyo kabla ya tarehe 8 Juni, 2022 yakionesha Jina, Namba ya ajira, Mahali anapoishi na Namba ya simu ya mlalamikaji. Malalamiko hayo yawasilishwe kupitia anwani ifuatayo:

**Katibu Mkuu,**
**Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu,**
**S. L. P. 2890.**
**Mji wa Serikali Mtumba,**
**Dodoma.**

**Au**
**Barua pepe: ps@kazi.go.tz**

IMETOLEWA NA KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU - KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU.

# Mbunge ataka utumbuaji MSD hadi madereva

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, ameitaka serikali kuhakikisha Bohari Kuu ya Dawa (MSD) inafumuliwa ipasavyo hadi madereva badala ya kuitazama menejimenti peke yake.

Akichangia juzi makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2022/23, Chikota alisema wafanyakazi wa kati wana uwezo wa kumkwamisha mkurugenzi wa taasisi.

"MSD wanasambaza dawa ukiona kama kuna madereva wanaotaka kukwamisha utendaji kazi ana uwezo wa kumwambia ofisa utumishi. Huyu ni CEO wa nane kwenye hii taasisi, kufumuliwa kwa MSD kusiwe ni kwa bodi na menejimenti pekee, twende hadi madereva na watumishi wa kati," alisema.

Alieleza kuwa lengo ni MSD itekeleze majukumu yake ipasavyo, akimpongeza Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu kwa kutoa takwimu za kweli kuhusu hali ya upatikanaji wa dawa ambayo kwa sasa ni asilimia 51.

"Nakupongeza waziri maana huko nyuma tulikuwa tukiletewa takwimu lakini kuhalisia hazikuwa za kweli, umeona badala ya kuwadanganya Watanzania umeamua kusema ukweli," alisema.

Kuhusu upotevu wa dawa, Chikota alitaka udhibitiwe, akisisitiza: "Bajeti ya MSD inapaswa kuongezwa na tulifanya marekebisho ya sheria kwamba wanaweza kujenga viwanda vya dawa, wa mradi pale Keko ambao unahitaji mtaji ili wazalishe dawa zenye ubora na kuuza nchi jirani.

"Changamoto hii ni kubwa sana hasa tunapokwenda maeneo ya vijijini. Kwa mfano, katika jimbo langu la Nanyamba kuna upungufu wa asilimia 79 kuna mahitaji 425, waliopo 106 tu naomba tutoe kibali maalum, kituo kama Majengo hakuna, madaktari hakuna, wauguzi tu ndio wanaotoa huduma, hii ina madhara makubwa sana," alionya.




Balozi wa China hapa nchini, Chen Mingjian, akizungumza wakati wa warsha ya kuadhimisha miaka 100 ya Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere iliyofanyika katika ubalozi huo, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: UBALOZI WA CHINA**

# China yaadhimisha miaka 100 ya Nyerere

**Na Mwandishi Wetu**

UBALOZI wa China nchini kwa kushirikiana na Taasisi ya Mwalimu Nyerere (MNF), umefanya kongamano kuadhimisha miaka 100 ya kuzaliwa kwa Mwalimu Julius Nyerere.

Kongamano hilo lililofanyika juzi jijini Dar es Salaam, ni sehemu muhimu ya mfululizo wa matukio ya kumbukumbu ya miaka 100 ya kuzaliwa kwa mwasisi huyo wa taifa la Tanzania.

Tukio hilo lilivuta hisia nyingi kutoka duru mbalimbali nchini Tanzania na vyombo vya wanadiplomasia nchini. Kongamano hilo lilihudhuriwa na zaidi ya watu 70.

Miongoni mwa waliohudhuria ni pamoja na mwakilishi wa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hamza Hassan Juma na Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana.

Wengine ni aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu wa Tanzania, Jaji Joseph Warioba na wawakilishi wa vyama vikuu vya siasa, vikundi vya kidini, jumuiya ya wafanyabiashara, taasisi za misaada na vyombo vya habari nchini Tanzania, familia ya Mwalimu Nyerere na mabalozi kadhaa na makamishna wakuu wa nchi za kigeni nchini Tanzania, jumla ya watu 70 walihudhuria katika kongamano hilo.

Katika ya kuwakaribisha waalikwa, Joseph Butiku, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya MNF, alisema Nyerere anapaswa kukumbukwa kama mtu mwenye kanuni na imani thabiti.

"Aliamini katika ubinadamu, haki za binadamu, na haki za watu binafsi na jamii. Aliamini katika amani na umoja," alisema Butiku.

Chen Mingjian, Balozi wa China nchini Tanzania, katika hotuba yake ya ufunguzi, alisema Nyerere ameweka hali ya urafiki wa kina na thabiti kati ya China na Tanzania, akajenga utamaduni wa kugawana dhiki na shida kati ya nchi hizo na kudhihirisha uadilifu wa China na Tanzania kwa jitihada zake za kujitegemea na kutoogopa madaraka.

Alisema Nyerere alidhihirisha ushirikishwaji na dira ya kimataifa ya China na Tanzania na kwamba urithi wake bado unaongoza maendeleo ya uhusiano kati ya China na Tanzania.

Balozi Chen alisisitiza kuwa China na Tanzania zinapaswa kurithi utajiri wa thamani wa kiroho wa Nyerere, kuongeza kasi ya kubadilishana uzoefu katika utawala, kuchochea uwezekano wa ushirikiano wa kiutendaji, kuimarisha msingi wa urafiki, kutetea haki kimataifa ili urafiki kati ya China na Tanzania uweze kustawi na kuzaa matunda kwenye udongo wenye rutuba uliolimwa na Nyerere.

Deng Li, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa China, alitoa ujumbe wa video katika kongamano hilo akisema Nyerere alipendwa sana na watu wa Tanzania, alifurahia heshima kubwa barani Afrika na alikuwa anafahamika na kuheshimiwa na Wachina.

"Tunamkumbuka Nyerere kwa kuendeleza urithi wake wa ujasiri na ushupavu, kurejea historia ya urafiki, mshikamano na ushirikiano kati ya China na Tanzania na China na Afrika na kutayarisha mwelekeo wa mustakabali wa uhusiano kati ya China na Tanzania na China na Afrika.

"Tunapaswa kuendeleza moyo wa urafiki na ushirikiano kati ya China na Afrika uliopendekezwa na Rais Xi Jinping wa China kwenye Mkutano wa Nane wa Mawaziri wa Baraza la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC), kujenga jumuiya ya China na Afrika yenye mustakabali wa pamoja katika enzi mpya na kutekeleza kwa pamoja programu tisa za ushirikiano kati ya China na Afrika," alisema.

"Tunapaswa kulinda kwa uthabiti mamlaka yetu, uhuru na uadilifu wa eneo, kupinga utawala, siasa za madaraka na kuingiliwa na nchi za nje, kutetea haki yetu ya kujiendeleza kama watu wa usawa, na kukuza utaratibu mpya wa kimataifa wenye haki na usawa zaidi ili kuunda mustakabali bora wa China na Afrika," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Dk. Mwinyi, Waziri Hamza alisema Nyerere na mwasisi wa Zanzibar, Abeid Amani Karume, ndio waasisi wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulioanzishwa mwaka 1964 na kuanzishwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hamza aliongeza kuwa Nyerere alifundisha Watanzania kujitegemea na kuacha kutegemea misaada kutoka nje.

Washiriki wa kongamano hilo walikuwa na mijadala yenye mada tatu, ambazo ni Mwalimu Nyerere na Ukombozi wa Tanzania na Kusini mwa Afrika, Mwalimu Nyerere na Amani na Umoja wa Afrika, na Mwalimu Nyerere na China - Kiuchumi, Kisiasa na Mahusiano ya Kijamii.

Katibu Mkuu Mstaafu wa CCM, Wilson Mkama, Prof. Issa Shivji kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Mkurugenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Kichina USDM, Prof. Humphrey Moshi na wanajopo wengine walitoa mada zao na kubadilishana kwa kina maoni na washiriki waliokuwepo kwenye kongamano hilo. Jaji Warioba alitoa hotuba ya kuhitimisha kongamano hilo.

## Chuo chajitosa shida masomo ya sayansi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUKABILIANA na uhaba wa walimu na maabara za masomo ya sayansi na hisabati, Chuo Kikuu cha St. Joseph kimebuni mradi wa kusaidia jamii kufundisha masomo hayo (stem on wheels) ili kuongeza idadi ya wanafunzi wa sayansi nchini.

Mradi huo umetokana na utafiti mdogo uliofanywa katika Mkoa wa Dar es Salaam na kubaini kuwapo kwa uhaba huo unaosababisha kuwa na idadi ndogo ya wanafunzi wanaosoma sayansi.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Eliab Opiyo, akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kwenye maonyesho ya wiki ya ubunifu kwa mwaka 2022, alisema mradi huo unalenga kusaidia jamii kufundisha masomo ya Sayansi, Hisabati na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa shule zenye uhitaji.

Alisema wameajiri walimu kwa ajili ya kutoa huduma hiyo na kubuni gari maalumu lenye maabara za Sayansi na TEHAMA.

"Tunatekeleza mradi huu kwa namna mbili, tunatumia wanafunzi wetu waliohitimu kutoka St. Joseph na mpaka sasa tumeajiri 18 ambao wapo kwenye shule 18, wanasaidia kuchangia kwenye ufundishaji masomo haya.

"Kitu cha pili ni hii basi ambalo ni maabara, ina vifaa mbalimbali vya kufundishia masomo ya Sayansi na TEHAMA, uwezo wake ni kuchukua wanafunzi 20 ambao wanaweza kukaa kwa wakati mmoja na kuna vifaa mbalimbali kwa ajili ya maabara," alisema.

Makamu Mkuu wa Chuo wa Masuala ya Taaluma, Utafiti na Huduma kwa Jamii, Prof. Alfonse Dubi, alisema wamebuni mradi huo kusaidia jamii hasa kwenye shule zenye uhitaji na imetokana na utafiti waliofanya kwenye baadhi ya shule za Mkoa wa Dar es Salaam.

"Kuna shule hazina maabara, zingine hazina vifaa, zingine hazina walimu, hii basi tumeigeuza kuwa maabara yaani mobile laboratory, itakuwa inatembea kwenye shule na kufanya mafunzo kwa vitendo kwa masomo ya sayansi na TEHAMA, ndani ya gari kuna laptop, kuna maabara ya Fizikia, Kemia na Baiolojia," alisema.

Mmoja wa wahitimu wa chuo hicho ambaye ni mratibu wa mradi hiyo, Dickson Mathew, alisema mradi huo unasaidia wanafunzi wa masomo ya sayansi ngazi za sekondari kutokana na kuwa na idadi ndogo ya wanafunzi kwenye vyuo kwa kukosa msingi mzuri wa sayansi.

# Wanaopanga safu za uongozi CCM Dar wapewa angalizo

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Dar es Salaam, Adamu Ngalawa, amesema Halmashauri Kuu ya Mkoa imetoa onyo kali kwa viongozi wachache wanaopanga safu ya uchaguzi unaoendelea kufanyika nchini kote.

Vile vile, alisema viongozi watakaobainika kuhonga safu, kutumia fedha na kuhujumu uchaguzi wa CCM mwaka huu, watachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa kanuni za chama.

Kauli hiyo aliitoa jana jijini Dar es Salaam katika mkutano wake na waandishi wa habari akitoa taarifa ya mkutano mkuu wa Halmashauri Kuu ya Mkoa, uliokete Mei 16, mwaka huu, kwa lengo la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kutimiza ahadi ya kuongeza mishahara na kuitangaza nchi kupitia filamu ya Royal Tour.

"Tathmini ya awali halmashauri kuu imekemea vikali viongozi au wagombea wachache wanaopanga safu zao na kutumia fedha katika kushika nyadhifa mbalimbali na kwamba fedha sio msingi wa kushinda uchaguzi," alisema Ngalawa.

Mbali na kupanga safu, pia CCM Dar es Salaam imepiga marufuku wanachama wanaogombea nafasi mbalimbali kutoka wilaya moja kwenda nyingine, kila mgombea achukue fomu na kugombea eneo analoishi ama katika eneo lake.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Kate Kamba, alisema mkoa wake unampongeza Rais Samia kwa kuitangaza nchi na vivutio vyake na kuwaomba wawekezaji wajitokeze kujenga hoteli za kisasa kwa ajili ya kupokea watalii.

Kadhalika, aliwataka wakazi wa Dar es Salaam kujitokeza kwa wingi kwenda kuchoma chanjo ya UVIKO-19 kwa usalama wa wote.

"Halmashauri Kuu inampongeza Rais Samia kwa kuitangaza nchi kupitia filamu ya Royal Tour, kuwajali watumishi wa umma kwa kuwaongezea mishahara kwa asilimia 23," alisema Kate Kamba.

Pia walimshukuru Kamanda wa Kanda Maalum ya Polisi, Jumanne Muliro, kwa kuhakikisha ulinzi wa kutosha na kupambana na wahalifu na ushirikiano anaowapa katika suala zima la ulinzi na usalama.

## Machinga, wajasiriamali wapatiwa uwezeshwaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAMACHINGA na wajasiriamali wametangaziwa neema ya fursa ya huduma za kibenki.

Uwezeshaji huo unatajwa kuwa unalenga kurahisisha uendeshwaji wa biashara miongoni mwa wafanyabiashara wadogo na wajasiriamali wakiwamo mamalishe, bodaboda, mafundi, wauza maduka na makundi mengine kwa kuwawezesha kuweka akiba kwa urahisi, kupokea malipo kwa njia za kidijitali sambamba na kuyaunganisha makundi hayo na fursa mbalimbali za kibiashara ikiwamo mikopo.

Benki ya Exim ndiyo iliyotoa fursa hiyo kwa kuzindua huduma kwa wamachinga na wajasiriamali maalum kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo na wajasiriamali ijulikanayo kwa jina la 'Exim Wajasiriamali Akaunti' ikilenga kusogeza karibu na kuhamasisha huduma za kibenki kwa makundi hayo muhimu.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa bidhaa hiyo jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mkuu Idara ya Fedha Benki ya Exim, Shani Kinswaga alisema pamoja na mambo mengine, huduma hiyo inaunga mkono wito wa serikali unaozihimiza taasisi za kifedha nchini kubuni huduma mbalimbali zinazolenga kuwasaidia wajasirimali na wafanyabiashara wadogo hususani vijana na kinamama kujikwamua kiuchumi.

"Huduma hii mpya ni mwitikio wa maoni ambayo tumekuwa tukiyapokea kutoka kwa wadau wetu mbalimbali wakiwamo wateja wetu. 'Exim Wajasiriamali Akaunti' ni huduma inayowapa urahisi wafanyabiashara wadogo iwapo hawajasajiliwa BRELA wakiwa na leseni ya biashara au TIN namba kufanya malipo mbalimbali ikiwamo njia ya mtandaoni, njia ya kadi, njia ya hundi na hata njia za kuhamisha pesa kutoka benki moja kwenda nyingine," alisema.

Alisema huduma hiyo pia inakwenda sambamba na huduma ya Bima ya Maisha inayotolewa na benki hiyo.

Mkuu wa Bidhaa za Rejareja na Uhakika wa Mapato wa Benki hiyo, Mtenya Cheya, alisema huduma hiyo ni maalum kwa ajili ya wateja wa sasa wa benki hiyo pamoja na wateja wapya.



Ofisa Mkuu Idara ya Fedha Benki ya Exim, Shani Kinswaga (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa huduma mpya ya benki hiyo iitwayo 'Exim Wajasiriamali Akaunti' mahususi kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wajasiriamali. Kushoto ni Mkuu wa Bidhaa za Rejareja na Uhakika wa Mapato wa benki hiyo, Mtenya Cheya na Meneja Msaidizi wa Bidhaa za Rejareja, Callist Butunga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Utafiti wabainisha kasi ya ukuaji kampuni ya Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

RIPOTI ya utafiti ya 'Financial Times' imeitaja Kampuni ya Silverlands Tanzania kuwa ni miongoni mwa kampuni zinazokuwa kwa kasi barani Afrika.

Ripoti hiyo imezitaja jumla ya kampuni bora 75 barani Afrika kwa kuzingatia vigezo vya ukuaji mkubwa wa mapato kati ya mwaka 2017 na 2020.

Kampuni sita tu katika sekta ya kilimo ziliweza kuwa miongoni mwa kampuni hizo 75.

Kampuni ya Silverlands ni miongoni mwa kampuni mbili tu za Kitanzania zilizofanikiwa kuwa miongoni mwa kampuni bora 75 kwa kufanikiwa kuwa na ongezeko la mapato yake kwa asilimia 40.4, na hivyo kushika nafasi ya 25 kwenye nafasi hizo 75.

Kampuni imefanikiwa kukua kwa kiwango hicho hata katika kipindi kigumu cha athari za ugonjwa wa Uviko-19.

Kampuni ya Silver Street Capital, ambayo ni mshauri mkubwa wa masuala uwekezaji, kwa mara ya kwanza iliwekeza katika kampuni Silverlands Tanzania mwaka 2014 kwa dhumuni la kuleta matokeo chanya katika wafugaji wadogo wa kuku na wakulima wa nafaka katika nchi za Afrika Mashariki, sekta ambayo huko nyuma ilikuwa ina maendeleo ya kiwango cha chini.

Imejikita kwenye biashara ya kuku na kuzalisha vyakula na vifaranga vyenye ubora wa hali ya juu.

Kutoka mwaka 2014 mpaka sasa, Silverlands Tanzania imekua ni kampuni yenye uzalishaji mkubwa wa vyakula vya kuku Tanzania na pia ni ya tatu kwa uzalishaji wa vifaranga vya siku, ambapo iliuza vifaranga milioni 14 mwaka 2021.

Kabla ya Silverlands, sekta ya ufugaji kuku ilibaki kuwa ya chini kwa sababu ya kukosekana vifaranga vya kutosha na vyenye ubora.

Kampuni ya STL ilianzisha aina mpya ya kuku wa kisasa wa 'layers' na 'broilers' vile vile 'Sasso'.

Hatua hiyo ni katika kuleta aina ya kuku wa kisasa wanaofaa kwa mazingira ya vijijini.

Kuku na chakula kinachozalishwa na Silverlands Tanzania kinalewalenga wafugaji wadogo ambao huwakilisha kundi kubwa la wafugaji hapa Tanzania.

Kwa chakula bora na vifaranga, wafugaji wa kuku wanaweza kuzalisha kuku kwa faida na uhitaji umekuwa ukikua.

Kuongezeka kwa uzalishaji wa kuku na mayai kumesaidia kupunguza kwa utapio mlo kwa watoto, tatizo ambalo limeenea katika nchi za Kusini mwa Afrika.

Kampuni ya Silverlands Tanzania ilianzisha kiwanda cha kwanza cha kuchakata soya na hii imesaidia kufanya maharage ya soya kuwa kwenye mzunguko na mahindi kwa wazalishaji wadogo wa nafaka kuongeza upatikanaji kutoka hali ya awali.

Kampuni ya Silverlands Tanzania kwa sasa inanunua mahindi na soya kutoka kwa wakulima wadogo 29,000.

Kampuni ilianzisha na kuendesha vituo 19 vya usambazaji nchini kote vikiwa na wasambazaji wadogo wadogo wapatao 350 wanaouza bidhaa zake kwa wafugaji wadogo wa kuku wapatao 134,000, ambao asilimia 75 ni wanawake.

Kipato cha wakulima hao wadogo kimeongezeka kwa asilimia 50 kwa sababu ya kampuni ya Silverlands Tanzania.

"Tunajisikia faraja kwa ukuaji mkubwa wa kampuni ya Silverlands Tanzania nchini Tanzania kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita. Imeonyesha ni kwa namna gani biashara inaweza kutengenezwa kwa faida, kukua kwa kasi na kuwa na matokeo chanya katika jamii kwa kukuza vipato vya maelfu ya wakulima wadogo," alisema Dk. Ben Moshi, Mwenyekiti wa Silverlands Tanzania Limited.

Ofisa Mkuu wa Uwekezaji wa kampuni ya SilverStreet Capital, Gary Vaughan-Smith, alisema: "Uongozi wa Silverland Tanzania umefanya kazi ya kipekee kwa kuanzisha biashara yenye nguvu yenye ukuaji mkubwa nchini Tanzania, japokuwa kuna ugonjwa wa Uviko-19.

# Timu kupitia mkataba mpya wa Songas yaundwa

BUNGE limeelezwa kuwa serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) imeunda timu ya kupitia masuala ya msingi ya kuzingatiwa kwenye mkataba mpya na kampuni ya Songas ili usiwe na dosari kwa ajili ya maslahi kwa taifa.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, aliliambia bunge jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Jesca Kishoa.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali imejipangaje kuhakikisha kwenye mkataba huo mpya unakuwa hauna dosari kwa manufaa ya wananchi kwa mwaka 2024 ambao ndio mwaka wa mwisho wa mkataba wa makubaliano baina ya Kampuni ya Songas na serikali.

Akijibu swali hilo, Byabato alikiri kuwa mkataba kati ya serikali na Kampuni ya Songas utaisha muda wake Julai, 2024 na ili kuhakikisha serikali inakuwa na mkataba usiokuwa na dosari, serikali haitaongeza muda wa mkataba utakaoishia Julai, 2024.

"Baada yake, serikali itajadili mkataba mpya na iwapo pande zote zitakubaliana, mkataba mpya wenye tija kwa taifa na usio kuwa na dosari utasainiwa, tayari serikali kupitia TANESCO imeunda timu ya kupitia masuala ya msingi ya kuzingatiwa kwenye mkataba mpya kwa ajili ya maslahi kwa taifa," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji sababu za kusuasua kutekelezwa kwa sheria inayotaka mikataba yote ya uzinduaji kuwekwa wazi.

"Mkataba wa serikali na Songas wa mwaka 2004 unanyima fursa ya Tanzania kunufaika na rasilimali kikamilifu, je, serikali imejipangaje mwaka 2024 haifanyi makosa mbalimbali ikiwamo mgawanyo wa hisa?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Byabato alisema timu hiyo iliyoundwa itapitia mkataba uliopo ili kubaini dosari zilizojitokeza ili zisijirudie tena kwenye mkataba mpya.

"Ipo timu imeundwa na TANESCO inaendelea na ufuatiliaji na ipo timu imeundwa na wizara inaendelea na upitiaji, ipo timu imeundwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na tuna miaka miwili kufikia muda wa kuisha huu mkataba, hivyo itatupa muda wa kupitia ili tutakaoingia uzingatie maslahi ya taifa,"alisema.

Kuhusu uwazi wa mikataba, Byabato alisema serikali imekuwa ikiweka wazi mikataba ikiwamo kwenye kamati za bunge.

Kadhalika, katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum, Esther Bulaya, alisema Wizara ya Nishati ina tatizo la mikataba mbalimbali inayohusu umeme na kusababisha hasara kwa taifa.

"Hamuoni sasa ni wakati kama serikali kupitia mikataba yote ili kuona dosari zilizojitokeza, ili huko tunakokwenda nchi isipate hasara irekebishwe sasa hivi ikiwamo mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere," alisema.

Byabato akijibu swali hilo, alisema amelichukua na serikali itaangalia namna bora ya kupitia mikataba yote na ile iliyokwisha itafanya kuwa mizuri zaidi kwa maslahi ya taifa.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi, akijibu maswali yaliyoulizwa na baadhi ya wabunge kwenye kikao cha Bunge la Bajeti linaloendelea jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Vijana 12% wenye uwezo kufanya kazi hawana ajira

OFISI ya Waziri Mkuu, imesema vijana asilimia 12.2 wenye uwezo wa kufanya kazi, hawana ajira. Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji ni vijana wangapi hawana ajira nchini na serikali imewaandaaje kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi wa mwaka 2021 unaonyesha kuwa vijana wa umri wa miaka 15 hadi 35 ni 17, 712,831.

"Kati yao, vijana 14, 219,191 wana uwezo wa kufanya kazi na vijana 3, 493,640 hawana uwezo wa kufanya kazi kutokana na sababu mbalimbali kama vile masomo, ugonjwa. Kati ya vijana wenye uwezo wa kufanya kazi, vijana 12, 486,682 sawa na asilimia 87.8 wana ajira na vijana 1, 732,509 sawa na asilimia 12.2 hawana ajira,"alisema.

Hata hivyo, alisema katika kuhakikisha vijana wanaandaliwa ipasavyo kushindana katika soko la ajira la ndani na nje, serikali inatekeleza programu na mikakati mbalimbali ikiwamo mafunzo ya uanagenzi, mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa wahitimu.

Pia, alisema mafunzo ya urasimishaji ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo (RPL) na mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya vitalu nyumba.

"Kupitia mafunzo haya, zaidi ya vijana 84,245 wamenufaika. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu imeendelea kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kuboresha mafunzo mbalimbali ya elimu na ufundi ikiwamo zoezi la maboresho ya mitaala pamoja na Wizara ya Kilimo katika kuanzisha programu za mafunzo ya ujuzi katika kilimo ambacho kina uwezo wa kuajiri vijana wengi zaidi," alisema.

## Mbunge ataka fidia wananchi waliopitiwa na mradi wa umeme

MBUNGE wa Mbeya Vijijini (CCM), Oran Njeza, ameitaka serikali kuwalipa fidia wananchi wa Mbeya waliopisha mradi wa ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme wa Kilovolti 400 kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma, Sumbawanga, Mpanda hadi Kigoma.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alisema mradi huo ulitarajiwa kuwapatia umeme wananchi wanaopitiwa na umeme huo na kuhoji lini wananchi watapatiwa umeme.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alisema serikali kupitia Shirika la Umeme (TANESCO) inaendelea na maandalizi ya ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme mkubwa wenye msongo wa kilovolti 400 kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga yenye urefu wa kilomita 616.

Alisema mradi huo pia unahusisha ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Iringa, Kisada, Mbeya, Tunduma na Sumbawanga pamoja na ujenzi wa kilomita nne za njia ya umeme msongo wa kilovolti 400 kwenda kwenye mpaka wa Tanzania na Zambia.

"Uthamini unafanywa na TANESCO kwa kushirikiana na wathamini wateule wa Wilaya za Iringa, Mufindi, Mafinga, Mbarali, Mbeya, Jiji la Mbeya, Mbozi, Tunduma, Momba na Sumbawanga ambapo mradi unapita,"alisema.

Hata hivyo, alisema hadi kufikia Aprili, 2022 majedwali ya fidia ya Halmashauri za Iringa, Mufindi, Mafinga, Momba na Mbarali tayari yameshaidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali na kukabidhiwa TANESCO kwa ajili ya kuanza maandalizi ya malipo.

"Majedwali ya Wilaya za Mbeya, Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Mbozi, Tunduma na Sumbawanga yapo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji. Fidia hizi zinatarajia kuanza kulipwa mwaka wa fedha 2022/23," alisema.




Habari zote na Augusta Njoji

# ama

ALHAMISI MEI 19, 2022

AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

**DARASA LA TATHMINI**
**Kilivyo kitendawili cha matukio watoto wanaonajisiwa, afya zao**




Ukurasa 14

**MAPINDUZI MAKUBWA... Huduma 'M- Mama ' inavyowanusuru kinamama hatarini kipindi kujifungua**

# Kinga Polio yaanza kwa chanjo, safari miezi kadhaa hadi Julai

**Na Mary Geofrey**

CHANJO ya ugonjwa wa Polio kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano, imeanza kutolewa nchini kote jana Mei hadi Jumapili ijayo, tarehe 21.

Utoaji huo wa chanjo unakuwa kwenye mfumo wa kampeni itakayofanyika nyumba kwa nyumba, mtaa kwa mtaa, sokoni na maeneo ya mikusanyiko kwa lengo la kufikia watoto 10,567,805 wenye umri huo.

Ofisa Programu, Mpango wa Taifa wa Chanjo wa Wizara ya Afya, Lotalis Gadau, anasema kampeni hiyo itasaidia kuzuia kuenea ugonjwa huo, ambao una kawaida ya kushambulia viungo vya mwili, kusababisha ulemavu wa kudumu na kifo.

Anasema kampeni itafanyika kwa awamu tatu, kuanzia mwezi Mei, Juni hadi Julai ikiwahusisha wasimamizi wa kitaifa katika mikoa yote.

Gadau anasema, kampeni hiyo itahusisha makundi matatu ya wahamasishaji, watoa chanjo na wakaguzi wa kuhakiki kama kuna mtoto ambaye hajapata chanjo hiyo.

Anafafanua kuwa kila mtoto atakayepatiwa chanjo hiyo atawekewa alama ya wino kwenye kidole kidogo cha mwisho ambayo inafutika baada ya wiki, ili kuonyesha amepata huduma.

Iko bayana ugonjwa wa Polio kwa miaka mingi umekuwa tishio kwa nchi nyingi duniani ikiwamo Tanzania na kwa mara ya mwisho mgonjwa wa aina hiyo kupatikana nchini ni Julai mwaka 1996, kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Afya.




Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, alipozindua chanjo dhidi ya Polio. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Katika kipindi cha hivi karibu zilianza kuenea habari kuwa, nchi jirani ya Malawi ina mgonjwa wa Polio, aliyetangazwa Februari 17, mwaka huu.

Hivyo, kutokana na ujirani uliopo kati ya nchi hizo mbili na mwingiliano wa wananchi wake, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) limefanya tathimini inayoonyesha kuwa Tanzania ipo hatarini kupata maambukizi hayo, kutoka Malawi.

Imeonekana, maambukizi yanaweza kuchukua sura mpya, ikiwa hatua madhubuti hazitachukuliwa katika kuhakikisha serikali inadhibiti maambukizi husika.




Dawa ya chanjo ya Polio.

Kuna jambo linalofahamika katika nadharia ya Polio kwamba ni ugonjwa usio na tiba, isipokuwa tu unaweza kuzuiliwa kwa kupata chanjo ya matone au sindano na ndiyo sababu ya serikali kuanzisha chanjo ya ugonjwa huo kwa watoto wote nchini wenye umri chini ya miaka mitano.

Lengo ni kuwakinga watoto hao na maambukizi hayo, endapo itatokea ugonjwa huo umeingia nchini

**VIASHIRIA VYAKE**

Viashiria vya ugonjwa huo ni pamoja na ulemavu wa ghafla, kulegea kwa viungo, kukosa nguvu, kushindwa kunyanyua mguu au mkono, mtoto kushindwa kukaa, kushindwa kutembea na kuvuta miguu.

Kiafya, inahimizwa na wataalamu wa afya, pale inapotokea mtoto ameanza kupata dalili hizo na nyinginezo, anatakiwa kuwahishwa katika kituo cha afya kwa ajili ya matibabu, maana 'kinga ni bora kuliko tiba' na wazazi na walezi wanaaswa na serikali kuwajibika kuwa mstari wa mbele kuwatoa watoto wao kupata chanjo hiyo muhimu.

Hadi sasa kitaifa elimu ya kutosha kuhusu chanjo imeshatolewa, umuhimu na faida zake katika kuikinga afya ya mtu.

Mkakati wa Polio unasisitiza nia ya serikali kutimiza lengo lake la kutoa kinga kwa watoto, elimu inaanza kwanza kwa wazazi, walezi na wasaidizi wa kazi majumbani, ili kuwatoa watoto wapate chanjo.

Serikali imeandaa wataalam wa afya wa kutoa chanjo ya matone na wengine watakaoweka alama ya wino kwenye vidole vya mwisho vya watoto, ili watambulike kuwa wamepata chanjo.

Chanjo mara zote ni muhimu kwa watoto wadogo na kwa manufaa ya taifa letu, kwani afya binafsi ni sehemu ya mtaji wa maendeleo.

AFYA

DARASA LA TATHMINI

# Kilivyo kitendawili cha matukio watoto wanaonajisiwa, afya zao

**Na Pankras Luoga, MUHAS**




Watoto kutoka Shule mbalimbali za Dar es Salaam, katika picha ya pamoja na Rais Mstaafu, Ally Hassan Mwinyi na viongozi wengine wa serikali, katika maadhimisho Siku ya Haki ya Mtoto Duniani, katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Julius Nyerere. **PICHA: MTANDAO.**

KUMEKUWAPO ongezeko kubwa la taarifa za vitendo vya watoto kulawitiwa na kubakwa katika maeneo mbalimbali nchini, ikitoa ishara isiyofaa.

Hapo kunarejewa mwezi Februari mwaka huu, Jeshi la Polisi Mkoa wa Katavi lilitoa taarifa ya kumkamata mkufunzi wa kidini katika eneo lake kikazi la kiimani huko Mpanda, akituhumiwa kuwalawiti watoto na alipohojiwa anadaiwa alikiri kutenda vitendo hivyo.

Tukio jingine ni la mwezi uliofuata Machi mkoani Geita, kukaripotiwa Polisi ilikuwa ikimsaka kijana anayetuhumiwa kuwalawiti watoto watatu waliokuwa wakiishi na mlalamikiwa huyo, ambaye ni mjomba wao.

Jingine la namna hiyo likaripotiwa mwezi uliopita mkoani Iringa katika shule mojawapo ya sekondari, ikihusisha watoto zaidi ya 19 wanaodaiwa kulawitiwa.

Ni taarifa ambayo haikupishana sana na nyingine mwezi huo, ikihusu kulawitiwa watoto wanane katika shule moja ya msingi iliyoko Songea mkoani Ruvuma, tatizo lililogunduliwa na walimu kutokana na watoto hao kuomba ruhusa kila mara kwenda chooni.

Hata pale walimu walipoanza kuwahoji watoto hao kujua chanzo cha madhira hayo, walifikia kujua mkasa wa kuwapo kijana mtaani anayewafanyia vitendo hivyo, akiwahadaa kwa zawadi kama pipi, huku akifanya nao michezo ya kukimbizana.

Hapo kukaripotiwa kwamba mtuhumiwa huyo aliwatishia watoto hao kwamba angewadhuru iwapo wangetoa taarifa hiyo kwa mtu yoyote.

Pia, ikaelezwa kwamba wazazi wa watoto hao walipoulizwa kuhusu kuwapo vitendo hivyo vya udhalilishaji, walionekana kutokujua kuhusu kilichoendelea kwa watoto wao, licha ya kuwapo viashiria vya wazi kwa watoto tajwa.

Hivyo, vinajumuisha kwamba watoto hao kuwa na michubuko katika sehemu za siri, kupata maumivu makali wakati wa kujisaidia na kutembea kwa shida.

### NINI MZIZI WAKE?

Kwa sasa, katika jamii kumekuwapo tathmini na ufuatiliaji duni wa wazazi na walezi katika malezi ya watoto wao. Hii inatokana na kubadilika kwa mifumo ya maisha yenye sura ya 'kutingwa na majukumu' wakitafuta pesa na mahitaji, wakisahau ya familia na kusahau malezi na ulinzi wa watoto wao.

Hapo unatolewa mfano wa uhalisia pale wafanyakazi wa umma na binafsi, pia wafanyabiashara wapotingwa sana na majukumu hayo, hata kuishia kutumia muda mfupi kukaa na kuongea na watoto, wanapoteza ufahamu wa kutambua maendeleo ya mabadiliko na changamoto za watoto hao.

Hayo ndiyo mazingira halisi yanayochangia kuibuka madhara na matukio yasiyofaa kwa watoto na familia, kukishuhudiwa tabia ya kushinda na kukesha kwenye vibanda vya kuonyesha video na mpira.

Ni katika mustakabali huo, kumeshuhudiwa udhalilishaji, ulawiti, ubakaji, mimba za utotoni, kutohudhuria au kukatisha masomo, kujihusisha na ulevi, utumiaji dawa za kulevya, wizi na ujambazi.

### KINACHOJIRI NCHINI

Shirika la habari la kimataifa Februari mwaka jana likarejea ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), linalofafanua kuwapo mikasa na kesi nyingi visiwani Zanzibar ya udhalilishaji kingono.

Kwa mujibu wa utafiti uliotajwa wa UNICEF, kuna watoto wa kiume wanaokumbwa na madhila hayo, lakini kiasi kikubwa ni mabinti walio katika umri wa utotoni, hata kushinikiza hitaji la kidola serikalini Zanzibar, kuwapo sheria na mahakama maalumu inayohusiana na udhalilishaji.

"Tatizo kubwa visiwani hapa ni suala la muhali, muhali maana yake ni kutofanya jambo ambalo linastahiki kulifanya, lakini unaona tabu kulifanya, mfano aliyebaka ni baba kambaka mtoto, mama anakataa kumtoa baba kama mbakaji.

"Mjomba anataka kesi iende, lakini babu hataki kwa sababu aliyebaka ni mtoto wao, kwa hiyo changamoto ndio hiyo" akanukuliwa alipokuwa Mkuu Wilaya ya Mjini Unguja mwaka jana, Rashidi Msakara.

### ULINGO WA MIKASA

Kupitia ripoti za tafiti mbalimbali, kuna maeneo ambayo watoto wanapata udhalilishaji njiani wakitoka nyumbani kwenda shule na kurudi.

Baadhi ya walimu wa madarasa wamepatwa ama kuhusishwa na kesi za udhalilishaji kwa watoto. Sasa, Umoja wa Walimu wa Madarasa umeshitushwa kwa kuanzisha taasisi ya kutoa elimu kwa umma, ili kukomesha vitendo vya udhalilishaji wa watoto.

"Taasisi hii tulianzisha baada ya kuona kwanini walimu wa madrasa wanahusishwa na matukio haya na kweli baadhi wamekua wakifanya, kwa hiyo tukaona tuanzishe ili tutoe elimu kwa walimu, wanafunzi na jamii kwa ujumla kuhusu vitendo hivi," anaripoti mmoja wa viongozi wao.

Pia, kwa kiasi kikubwa kada ya waendesha bodaboda wanatajwa kuwa waharibifu wakubwa, hasa kwa mabinti wa sekondari wakitumia mwanya wa wanafunzi watokao maeneo ya mbali na shule.

Shirika la habari Ujerumani DW, Februari mwaka jana likalinukuu jeshi la Polisi nchini kwamba mwaka 2020 kumekuwepo matukio ya ukatili dhidi ya watoto 7388, huku miaka mitano kabla, 2015 kulikuwepo matukio 5,803 yaliyoripotiwa.

Mdau Anna Henga, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu Tanzania, anasema kukithiri huko kwa imani za kishirikina miongoni mwa wanajamii wanaosaka utajiri, maeneo yaliyomulikwa zaidi ni maeneo Kanda ya Ziwa,

Aidha, ripoti zote zinaonyesha mwaka 2020 kulikuwapo ishara mpya kuhofiwa ukatili kwa watoto unaofanywa na baina yao, hasa matukio ya ulawiti shuleni.

Sophia Temba, ni Ofisa Programu wa Jukwaa la Utu wa Mtoto, Kitengo cha Ulinzi wa Mtoto, naye mchango wake katika hilo mwaka jana, ananyooshea kidole mmomonyoko wa maadili kwamba unachangiwa sana na utandawazi katika jamii.

### NINI KIFANYIKE?

Kuna ushauri wa kisaikolijia na kijamii, kwamba, wazazi na walezi waimarishe tathmini na ufuatiliaji wa karibu kwa watoto ili kugundua mwenendo na mabadiliko yanayotokea katika maisha ya watoto wao.

Pia, mwenendo na mabadiliko kitabia ni muhimu, kabla ya kufikiwa madhara makubwa, hali inayowasaidia wazazi kusahihisha kasoro zao za ulezi, kabla hazijajengeka na kuwa tabia au mazoea.

Wazazi na walezi wanaelekezwa, kuhakikisha mtoto anapewa muda, nafasi, heshima, upendo na hamasa au moyo katika kila jambo jema analolifanya na kupata mahitaji mengine yote kama malazi, nguo na chakula.

Hiyo inatajwa kuendana na kuwafanya wazazi wahakikishe mtoto anacheza na kushirikiana na wenye tabia, hata naye akaangukia tabia njema.

Pia, kunatajwa kuchangia umuhimu kimantiki, ni katika suala la kufanyika tathimini na ufuatiliaji wa karibu kwa watoto, kugundua mienendo na mabadiliko yanayotokea katika maisha ya watoto wao.

Ugunduzi wa mapema wa mienendo na mabadiliko ya kitabia na kimwili kwa watoto, unatajwa kitaalamu inawasaidia wazazi kuchukua hatua stahiki za kurekebisha yasiyofaa mapema, kabla hayajajengeka na kuwa tabia na mazoea.

• ***Mwandishi ni Mhadhiri Msaidizi wa Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathimini ya Miradi ya Afya, katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili. Anapatikana kwa simu: + 255 757 645 746.***

MAZINGIRA

KUTOWEKA SAMAKI ZIWA RUKWA...

# Wakazi walilia mizimu na imani, wataalamu wanena ni mazingira

- Kila pande yang'ang'ania sayansi yake
- Mamba nao 'washughulikia' binadamu

**Na Ibrahim Yassin, Songwe**


Baadhi ya wavuvi wa Ziwa Rukwa wakiwa kazini.

MTU anapofika wilayani Songwe, kuna tarafa inayoitwa Kwimba penye Ziwa Rukwa, mahali kulikotajwa chanzo muhimu cha samaki.

Katika miaka ya karibuni, kumekuwepo uhaba mkubwa wa samaki hao, hata kuzua kiulizo cha sababu ya uhaba huo.

Hapo ndipo kunakoibuka mjadala rasmi na mjadala 'pori' kuhusu suala hilo. Nadharia iliyoko kutoka kwa wenyeji ni kwamba, upo ukiukwaji mkubwa wa kanuni sahihi ya kulinda ziwa lizalishe samaki kwa wingi, wakiwa wanaelekeza kidole chao kwa kinamama.

Wataalamu hao wa kisayansi wana hoja inayokinzana nao, wakiweka kando mtazamo huo wa wenyeji, hoja zao nyingi zikiangukia afya ya viumbe hao na utunzaji mazingira ya Ziwa Rukwa katika eneo hilo la mkoa wa Songwe.

Hoja za wenyeji zinaegemea mila na utamaduni, wakiwalalamikia kuoga ziwani, pia wanaoosha vyombo vyenye masizi ziwani, wakidai ndio chanzo cha kutoweka samaki katika Ziwa Rukwa.

Nipashe hivi karibuni imewashuhudia wazee wa mila katika kijiji cha Udinde, wakiendesha ibada maalum ya tambiko kuombea mizimu kurejesha samaki katika ziwa hilo, huku uchumi wa wananchi ukipungua.

**WAZEE WA MILA**

Chifu Simon Kawana, ni kiongozi wa mila wa eneo hilo, anayesema wameamua kufanya maombi maalum kwa mzimu ilioyochukua samaki, irejeshe nafasi zao, baada ya samaki kukimbia.

Anadai miaka ya nyuma, ziwa hilo lilikuwa mbali na makazi ya watu na wamelazimika kufanya tambiko bila ya kuchinja mbuzi au kondoo, kutokana na ukata wa fedha.

Hapo anaiomba serikali iwaunge mkono katika hilo, kuwasaidia wafanikishe, maana kila mahali pana taratibu na mila, hivyo inapaswa kudumisha mila zilizopo.

Faustin Kawala ni Katibu wa Wazee wa Mila katika eneo hilo, analalamika katika kile anachokifafanua kwa maoni yake, wanawake kuoga na kufanya shughuli za kibinadamu kwenye maji, mizimu tajwa inachukia.

Pia, sababu nyingine anaitaja ni kuwepo uvuvi unaoitwa 'katuli' yaani kupiga maji na rungu kukimbiza samaki na kupatia majibu sasa ndio wanafanya tambiko maalum.

Maria Aliseni, mke wa mzee huyo wa mila, anawataka wazee wa mila waongeze jitihada za kutii mila yao, ili iendane na mwelekeo wa kitambiko.

Mzee Godfey Mwaulambo, anasema toka enzi za mkoloni kulikuwepo matambiko yaliyofanyika kwenye Mlima Kwimba na wao wamebaini kukiukwa mila zao, pia kanuni za kimazingira kwenye kingo za maji.

"Serikali iwasikilize wazee wa mila na kuwasaidia, wingi wa mambo ya kisasa (utandawazi), pia wingi wa mamba kuliko idadi ya samaki nayo ni sababu," anasema Mzee Mwaulambo na kuendelea:

"Mamba mmoja anazaa watoto 200 na wote hao chakula chao ni samaki, inafikia hatua wanakamata watu pembezoni mwa ziwa kwa ajili ya njaa."

**VIONGOZI WA SERIKALI**

Mwenyekiti wa kitongoji cha Iboma, kijiji cha Udinde,Andrea Kibwana, anawataka wazee wa kimila wasipuuzwe hoja zao, akirejea mwaka 1980 samaki katika ziwa hilo zilikuwa ni mboga tegemeo kwa wananchi, lakini sasa wametoweka.

Anaiomba serikali ishirikiane na wazee hao wa kimila kuondoa hali hiyo, akikumbusha hata Mlima Kwimba kulikofanyika matambiko, sasa umevamiwa na wafugaji, akilalamika palikuwa mahsusi wakazi kutambikia, pia wananchi jirani kutoka Sumbawanga.

**WATENDAJI SERIKALINI**

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Udinde, Ernest Mwankenja, anakiri samaki Ziwa Rukwa wametoweka, hali inayowakosesha mapato na kufanya vijana wengi kukimbilia Sumbawanga ambako samaki wanapatikana, ikididimiza nguvu zao.

Anasema mwaka jana, kata ya Udinde iliongoza kwa mapato katika kata zote za Halmashauri ya Songwe, tegemeo kubwa lilikuwa ziwa, ila sasa samaki hakuna na wamebaini shida iko katika uvuvi haramu kutumia vyandarua, katuli na makokoro.

Katika hilo anashauri ili kudhibiti hilo, serikali inapaswa kupandikiza samaki wapya kukabiliana na uhitaji wa wakazi wa ziwa hilo

Anasema, miaka ya nyuma wananchi wa Katavi na Sumbawanga pamoja na wa tarafa ya Kwimba, Songwe, walivua samaki ziwani upande uliochukuliwa na kuwa sehemu ya Hifadhi ya Taifa; ambayo ndiyo yenye samaki wengi.

Mwankenja anataja baadhi ya vitongoji husika kuwa sehemu ya hifadhi: Mluma, Mkamba, Mani, Yeye, Lwika, Kipanga, Mchangani, Jiwe la Msama, Mpai na Mtakuja.

Viongozi wengi, akiwemo mbunge Philipo Mulugo, wanaomba serikali iachie maeneo hayo, ili wananchi wavue na kuendesha maisha yao ya kila siku, na serikali kupata mapato.

Ofisa Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, Joel John, anasema kutoweka samaki Ziwa Rukwa, kumetokana na uharibifu wa mazingira kwa wavuvi wanaotumia zana zilizokatazwa na wamekuwa wakikabiliana na hilo.

Anasema kwa miaka miwili iliyopita, walikuwa wanakusanya tani 91,000 za samaki na kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, Sh. Milioni 91, lakini mwaka huu wa fedha samaki waliopatikana ni tani 19, 000 pekee na hata halmashauri yao kuambulia Sh.Milioni 19 pekee.

Ofisa Maliasili wilayani Songwe, Abdallah Mgonja, anafafanua kwamba, kutokana na wingi wa mamba Ziwa Rukwa, serikali ilijenga uzio wa chuma kudhibiti wananchi wasiliwe na mamba pindi wanapochota maji pembezoni mwa ziwa hilo, baada ya kuwepo mikasa mingi ya watu kuliwa na mamba.

Anasema, Rukwa ni miongoni mwa maziwa yenye mamba wengi, lakini tayari jitihada za serikali kutaka kuvuna na kuwapunguza zinafanyika, akiwataka wananchi wachukue tahadhari, wakati serikali ikichukua hatua.

Abraham Sambila, ni Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, anaungana na hoja samaki wametoweka na wao halmashauri wanajipanga kuhakikisha wanadhibiti uvuvi haramu na utunzaji mazingira, ili kurejesha samaki ambao ni chanzo muhimu cha mapato yao.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Songwe, Abdulkadir Mfilinge, anasema ushuru upatikanao ziwani humo ni muhimu kwao, huku Mbunge wa jimbo hilo Mulugo, anasema tayari serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuvuna mamba.

Pia kuhusu uzio wa chuma, anasema ukijengwa kudhibiti maafa kuhusu suala la uhaba wa samaki watu wa idara husika watashughulikia wakati yeye akiendelea kuiomba serikali kuhusu upandikizwaji.


Wazee wa Mila katika picha ya pamoja, baada ya kumaliza kuombea mizimu, samaki waongezeke ziwani. **PICHA ZOTE: IBRAHIM YASSIN.**

AFYA

MAPINDUZI MAKUBWA...

# Huduma 'M- Mama' inavyowanusuru kinamama hatarini kipindi kujifungua

## •'Vichanga' nao wameneemeka uhai



Dereva Edmund Kinubi, mkazi wa Tinde wilayani Shinyanga, anaye hudumia usafiri wa dharura wa M-Mama. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU.**

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

HUDUMA ya kitaifa ya usafirishaji wa dharura kwa wanawake wajawazito na watoto wachanga kuwahi kwenye huduma za afya na kupata matibabu 'M-Mama', imetoa ishara ya tija, zaidi vijijini, ambako asilimia kubwa wako mbali na huduma za afya .

Hapo kunatajwa umbali wa kati ya kilomita tano hadi 15 na huwa inapofikia kipindi cha wajawazito kujifungua, hupata changamoto ya usafiri kwenda kujifungua na mara nyingi hutumia usafiri wa bodaboda ambao siyo rafiki kwa mjamzito.

Ni ishara inayokumbusha malengo ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAMA), iliyoanza mwaka 2008, ikitaka kila kijiji kuwa na zahanati, kata kuwa na kituo cha afya, ngazi ya wilaya hadi juu, hospitali.

Huduma ya usafirishaji wa dharura wajawazito na watoto wachanga inatolewa bure, ikigharimiwa na serikali kwa kutumia magari ya watu binafsi vijijini, ambayo huwa rafiki kubeba wajawazito wanaoenda kwenye huduma za afya kujifungua salama.

### AFUNGUKA ILIVYOMUOKOA

Judith Kayegeji, anayeishi Usanda wilayani Shinyanga, ni mama wa watoto wawili, anasimulia 'M-Mama' ilivyookoa maisha yake wakati wa kujifungua katika Zahanati ya Usanda, mjini Shinyanga.

Anasimulia, baada ya kutokwa na damu nyingi, kukawepo ulazima kuhamishiwa Hospitali ya Rufani Shinyanga, katika mazingira ambayo hapakuwapo gari la wagonjwa.

Mama huyo anasema, alipofika kujifungua katika zahanati ya Usanda mwaka 2017, akaanza kutokwa damu nyingi na bahati mbaya hapakuwepo gari la kubeba wagonjwa, hali yake ilipokuwa mbaya, wakapiga simu kuomba huduma ya 'M-Mama' hata ikafika na kunusuru.

"Ukiangalia mazingira ya zahanati zetu huku vijijini, kupata huduma ya gari la wagonjwa kwa uharaka ni vigumu, hadi litoke Shinyanga mjini, tayari unakuwa umeshapoteza maisha," anasema Kayegeji.

"Baada ya hali yangu kuendelea kuwa mbaya, ndipo tukapiga simu kuomba huduma ya 'M-Mama', dereva alikuja haraka na kunipeleka hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga nikafika kwa wakati na kupata matibabu na kuokoa maisha yangu na mtoto," anaeleza.

Leo anaisifu huduma hiyo kwa kuokoa uhai wa wajawazito wengi na hasa vijijini, akidokeza manufaa yake ni huduma ya bure. Anaendelea: "Tofauti na kubebwa kwenye gari la wagonjwa (ambulance), ambayo yenyewe unagharamia usafiri na ukiwa huna pesa huduma yake inakuwa ya shida."

### DEREVA WA MRADI

Edmund Kinubi ni dereva kwenye mfumo wa 'M- Mama', anayesafirisha wajawazito, anasimulia namna ameokoa maisha ya wajawazito wengi aliowakuta katika hali mbaya kwa kuwawahisha penye matibabu.

Dereva Kinubi anasema, tangu alipoanza kutoa huduma hiyo ya usafiri mwaka 2019, ameshaokoa maisha ya wajawazito wengi, akifafanua afanyavyo kazi huwa anapigiwa simu na kufika haraka penye uhitaji, anamchukua mjamzito na kumuwahisha hospitalini anakohitajika kujifungua.

"Huku vijijini huduma za afya huwa zipo mbali sana na makazi ya wananchi. Kwenye ngazi ya zahanati huwa hakuna gari la wagonjwa (ambulance) na vijijini zahanati ndiyo nyingi, hivyo utoaji huduma hii ya usafiri imekuwa msaada mkubwa kwao.

"Zamani nilikuwa nafanya biashara ya kusafirisha abiria wakati nikiendelea na utoaji wa huduma hii ya 'M-Mama ya usafirishaji wajawazito, lakini baada ya kuona wengi wapo katika hatari ya kupoteza maisha, nikasitisha biashara ya kusafirisha abiria na kubaki kutoa huduma hii hadi sasa.

"Huduma hii ya kusafirisha wajawazito ina hitaji moyo wa huruma na kujitoa sana. Hapa Tinde tulikuwa madereva sita ambao tunatoa huduma hii, lakini wengine wote wameacha na kubaki peke yangu.

"Sababu nimeguswa na wajawazito wanavyoteseka kwa kukosa usafiri na kubebwa kwenye bodaboda usafiri ambao siyo salama kwao," anasimulia Kinubi.

### MUUGUZI MKUU SHINYANGA

Muuguzi Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Flora Kajumulla, anaelezea 'M-Mama' imesaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto mkoani humo, kutokana na uzazi.

Anafafanua mfumo wa rufani kutoka Wizara ya Afya, magari ya wagonjwa huwa hazifuati mgonjwa nyumbani, bali mgonjwa anatolewa kwenye Zahanati au kituo cha afya na kupelekwa kwenye hospitali kubwa kupatiwa matibabu zaidi.

Anasema katika mfumo 'M-Mama' mgonjwa anapiga simu bure kupitia namba zilizotolewa na anawasiliana moja kwa moja na watoa huduma au madereva waliopo kwenye mfumo huo na kisha wanafuatwa na gari hadi nyumbani, kupelekwa kwenye huduma ya afya kupata matibabu.

"Tofauti ya huduma ya M-Mama na za kawaida, huduma hii yenyewe inamfuata mgonjwa nyumbani kwake kupitia magari ambayo yameingizwa kwenye mfumo wa huduma hii ambayo yapo huko huko kijijini na kumsaidia mjamzito kufika kwenye huduma za afya kwa wakati," anaeleza Kajumulla.

"Huduma za kawaida magari ya wagonjwa (ambulance) yenyewe hayafuati mgonjwa nyumbani, bali anatolewa kwenye zahanati au kituo cha afya na kupelekwa kwenye hospitali kubwa," anaongeza.

Anataja tangu huduma hiyo ianze kazi mkoani Shinyanga mwaka huo 2017, kuwa hadi kufika mwaka jana wameshawafikia kinamama 5,769.

"Mwaka 2016 vifo vya mama vitokanavyo na uzazi vilikuwa 74, lakini baada ya kuanza huduma hii ya M-Mama mwaka 2017 na hadi kufikia mwaka jana (2021) tulipunguza vifo na kutokea 50 sawa na upungufu wa asilimia 40," anafafanua muuguzi huyo, anayesimamia mradi.

"Vifo vya watoto wachanga mwaka 2016 tulikuwa na vifo 1,080, lakini mwaka jana (2021) kutokana na huduma hii ya M-Mama vimepungua na kutokea 665 sawa na asilimia 45,"anaongeza.

### KAULI YA RAIS SAMIA

Mnamo Aprili 6 mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, wakati anazindua mfumo wa 'M-Mama' jijini Dodoma, kwa tafsiri ya kuhudumu kitaifa, akasema unatoa huduma ya dharura kusafirisha wajawazito na watoto wachanga kwenye huduma za afya.

Rais Samia anasema serikali itaendelea kuhakikisha maeneo yote yanakuwa na magari ya kubeba wagonjwa kufikia ngazi walau kila kata kuwa na gari moja.

"Tumeagiza 'ambulance' 233 za kawaida ambazo zitamwagwa Tanzania nzima, pia tumeagiza 'ambulance' 25 ambazo ni 'advance'. Hizi ni kama ngazi ya rufani kama zinakuwa hazitoshi au hazina vifaa basi hizi 25 zitatumika, pia tumeagiza magari 242 ya uratibu," anasema Rais Samia.

"Matumaini yangu ni kwamba magari na ambulance hizi zitakwenda kuongeza nguvu kwenye huduma hii ya M-Mama, ili kuwawahisha watoto na kina mama wajawazito hospitali,"anaongeza Rais Samia, aliyezoeleka pia kwa jina 'Mama'.

Mfumo huo wa 'M-Mama' ulianza kwa majaribio wilayani Sengerema mkoa wa Mwanza na Mkoa wa Shinyanga, ambako umeshawahudumia wanawake na watoto 12,000 kwa mafanikio ya kupunguza vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi.



Muuguzi Mkuu Mkoa wa Shinyanga, Flora Kajumulla, anayesimamia mradi wa M-Mama mkoani humo.

## JKT kutumika katika kutoa mafunzo kwa maofisa ugani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema wizara imejipanga kutumia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kutoa mafunzo ya nidhamu kwa Maofisa Ugani nchini ili kuleta heshima kwenye sekta ya kilimo.

Bashe alibainisha hayo jana kwenye kikao kazi cha Maofisa hao nchini kilichofanyika jijini hapa.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni pamoja na kutaka kuleta nidhamu na uwajibikaji katika kilimo kama JKT wanavyofanya katika uendeshaji kilimo cha mazao mbalimbali.

"Msishangae kuona leo tumewaita JKT hapa tuna mpango wa kushirikiana nao kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa Maoafisa Ugani ya nidhamu kwenye kilimo na wataalaamu wa kilimo watatoa mafunzo ya kilimo kama ilivyo ada," alisema Bashe.

Alisema wanafanya hivyo kwasababu sekta hiyo inasimamia usalama wa nchi kwenye suala la chakula kwa jamii hivyo ni lazima nidhamu iwapo.

Waziri Bashe alisema watapatiwa Vishkwambi ambavyo vitawasaidia kutoa taarifa za masuala ya kilimo kwa haraka, ikiwamo pale inapotokea taarifa ya hofu ya uwapo wa viwavijeshi kwenye maeneo yao.

"Vishkwambi vitasaidia kutoa taarifa kwa haraka tofauti na Ofisa Kilimo ambaye anatoa taarifa kwa maandishi itachelewa kufika kwa haraka sehemu husika," alisema Bashe.

Kuhusu skimu za umwagiliaji, alisema kuanzia Julai Mosi mwakani skimu zote zitaanza kusimamiwa na wizara na kuwataka maofisa hao kuwajibika kuzitembelea ili kuzitambua na kuongeza mapato ya fedha za skimu yataingizwa kwenye mfuko wa Hazina.

Bashe aliishukuru serikali kutokana na kuongeza bajeti kwenye huduma za ugani kutoka Sh. milioni 600 hadi Sh. bilioni 15.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa kilimo, Anthony Mavunde, alisema unahitajika ushirikiano wa pamoja ili kufikia malengo yaliyowekwa ya sekta hiyo ikue kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

Awali, Katibu Mkuu wizara hiyo, Andrew Massawe alisema hadi sasa wametoa mafunzo kwa Maofisa Ugani 2,886 na wakulima viongozi 870 na kutoa vitendea kazi.

# Vyuo elimu ya juu vyatakiwa kujiimarisha kiutafiti ubunifu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imevitaka vyuo vya elimu ya juu nchini kujiimarisha katika utafiti ili kupata maendeleo kwenye ugunduzi na ubunifu wa teknolojia zitakazosaidia Tanzania kupiga hatua zaidi kama zilivyo nchi za China na India.

Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, alitoa agizo hilo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua maonesho ya wiki ya ubunifu yanayokwenda sambamba na Mashindano ya Ubunifu wa Sayansi na Teknolojia (MAKISATU) kwa mwaka 2022 ambayo yameandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo(UNDP), kupitia mradi wake wa FUNGUO.

Alisema vyuo vikuu kazi yao ya msingi ni utafiti na kutaka kujiimarisha kwenye eneo hilo na kuwa na sera bora za utafiti ambazo zitasaidia na kuchagiza wabunifu na wagunduzi mbalimbali kwa kulinda haki zao na kufaidi matunda ya kazi zao.

Aidha, alitoa wito kwa wizara hiyo kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za Tanzania Bara na Zanzibar kuandaa mikakati maalum ya kulinda kazi mbalimbali za ubunifu.

"Kwa sababu dunia kila kitu siku hizi kimekuwa kijanja na ujanja mkubwa umekuwa ni kuchukua kazi za wengine, nchi mbalimbali zimepata maendeleo makubwa kwa sababu ya kuwa na mikakati madhubuti ya kulinda kazi za wabunifu, kwa hiyo ni vyema kuwasaidia na kuwa na mikakati ya kuwasaidia kujua namna gani na hatua gani za kulinda kazi za ubunifu, kwa kuwa bila kuzilinda zitakuwa hazina maana watavuja jasho lakini hawatapata tija ya jasho lao," alisema.

Alisema malengo ya serikali ni kuibua ubunifu na teknolojia ambazo zitachangia kuongeza kasi na kuleta ufanisi kwenye utoaji huduma pamoja na uzalishaji bidhaa.

Alitoa wito kwa wananchi kuhamasisha kushiriki katika kuonesha vipaji walivyobarikiwa na kuweka mkazo kwenye matumizi ya teknolojia mbalimbali.

"Matarajio ya serikali ni kuwa ubunifu na teknolojia zinazoibuliwa na wabunifu na wagunduzi nchini, zitaongeza tija katika uzalishaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda, kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa pamoja na kuboresha na kurahisisha utoaji wa huduma katika nyanja mbalimbali," alisema.

Kadhalika, alisema serikali zote mbili zimeazimia kujenga uwezo wa ndani wa kuendelea kuwekeza katika rasilimali watu, miundombinu na vifaa vya kisasa vya utafiti na ubunifu pamoja na kuimarisha mahusiano kati ya Taasisi za Sayansi na Teknolojia na sekta ya viwanda.

Kwa upande wake, Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda, alisema wabunifu 862 walijisajili kwa mwaka huu na wabunifu 86 bunifu zao zitashindanishwa ili kupata washindi.

Alisema kwenye wiki hiyo taasisi mbalimbali 50 zimeshiriki kwenye maonesho hayo pamoja na wabunifu 26 ambao bunifu zao zimefikia hatua ya kuingia sokoni na kuanza kutumika.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (katikati), akipiga makofi wakati wa ufunguzi wa kikao cha maofisa ugani kutoka mikoa yote nchini, jijini Dodoma juzi. Kulia ni Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Andrew Massawe. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

## Mikakati viashiria hatarishi sekta ya uvuvi yaandaliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeanza kuandaa daftari la viashiria hatarishi kwenye sekta ya uvuvi ili kuviwekea mkakati wa kuvidhibiti.

Kaimu Katibu Mkuu Sekta ya Uvuvi, Amosi Machilika aliyasema hayo jana kwenye mkutano wa wadau wa sekta hiyo uliofanyika jijini hapa.

Alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2010 katika sura 348.

"Lengo la kuandaa daftari la viashiria hatarishi ni kuiwezesha Sekta ya Uvuvi pamoja na wadau wake wanaotekeleza sera, mipango, mikakati na programu mbalimbali za kisekta kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa kiwango kikubwa kwa sababu viashiria hatarishi vitakuwa vimewekewa mikakati ya kudhibitiwa kabla ya kutokea na kukwamisha juhudi za sekta," alisema.

Machilika alisema kuwa matarajio ya sekta hiyo kwenye warsha hiyo ni kuwawezesha washiriki kupata uelewa mpana kuhusu viashiria hatarishi, kuvichambua kwa umakini na kuviwekea mikakati ya kuvidhibiti au kuviepuka ili kufikia malengo ya sekta hiyo.

"Sekta ya uvuvi imekuwa kwa asilimia 2.5 ambapo mchango wake kwenye pato la taifa ni asilimia 1.8 ikilinganishwa na asilimia 1.7 ya mwaka 2020," alisema.

Naye, Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali Msaidizi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Abraham Msechu, alisema daftari hilo linatakiwa kutumika na si kuishia kuliandaa.



# Sababu wakulima kahawa kunufaika

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA wa kahawa mikoa ya Mbeya, Songwe na Ruvuma wameanza kunufaika baada ya serikali kwa kushirikiana na wadau wanaohusika na mnyororo wa thamani wa zao hilo kufanya jitihada za kulipa thamani ndani na nje ya nchi.

Jitihada hizo zimezaa matunda ambapo kwa sasa wakulima wanauza kilo moja kwa Sh. 6,500 hadi 7,500 kutoka Sh. 4,300.

Baadhi ya wakulima walisema licha ya vikwazo wanavyokabiliana navyo katika uzalishaji lakini kupanda kwa bei ya kahawa kumeleta faraja kwao.

Grina Kalonge kutoka Chama cha Ushirika cha Lubanda AMCOS wilayani Ileje mkoani Songwe alisema ongezeko hilo la bei limechangiwa na wadau wanaohusika na mnyororo wa kahawa kuwapatia mbinu za uzalishaji ulio bora.

Kalonge alisema kwa sasa ameweza kumudu gharama za maisha ikiwamo kusomesha na kuongeza uzalishaji baada ya kupata fedha za kutosha kuendesha maisha yake.

Said Mwashozya kutoka Chama cha Ushirika wa Wakulima Igale Amcos iliyoko mkoani Mbeya alisema miongoni mwa wadau waliowasaidia wakulima kupata fedha nzuri kupitia zao hilo ni Shirika lisilokuwa la kiserikali la Cafe Africa Tanzania ambao licha ya kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara namna bora ya kuzalisha zao hilo, lakini pia wamewasaidia kutafuta masoko ili kunufaika.

"Hali ya sasa kwetu wakulima ni tofauti na ilivyokuwa kwa miaka mitatu iliyopita, tumeweza kuzalisha kwa tija na kupata soko la uhakika ambapo kwa kilo moja ya kahawa sasa tunauza kwa Sh. 6,500 hadi 7,000 kutoka 4,300 hali inayotusaidia kujikwamua na umaskini kupitia zao hilo," alisema Mwashozya.

Meneja Programu kutoka Shirika la Cafe Africa Tanzania, Samora Mnyaonga alisema wakulima, maofisa ugani na wadau wengine wanaohusika kwenye mnyororo wa thamani wa zao hilo kutoka mikoa ya Mbeya, Songwe na Ruvuma wamekutana mkoani Mbeya kujadili kwa pamoja masuala ya masoko, uongezaji thamani wa zao la kahawa pamoja na kuhimiza ushirikishwaji wa wanawake na vijana katika uzalishaji wa kahawa.

Mnyaonga alisema kupitia kikao hicho cha siku mbili kinatoa fursa ya kujadiliana na kutafuta fursa za masoko sambamba na kufundishana mbinu bora za uzalishaji wa zao hilo.

"Cafe Africa tunajivunia kuona bei ya zao la kahawa sasa imepanda na wakulima wetu wanafurahia kilimo hicho, tumekuwa na jukumu kubwa la kuwafundisha wakulima mbinu bora za kilimo mara kwa mara pamoja kuwatafutia masoko licha ya kuwa bado tuna kazi kubwa ya kuhakikisha zao la kahawa linakuwa kilimo cha wakulima wetu katika kujikwamua kiuchumi," alisema Mnyaonga.

Ofisa Ubora Mwandamizi wa zao hilo Kanda ya Mbeya, Gerald Mlay, alisema kwa sasa ubora wa zao la kahawa umeongezeka na kusaidia bei kupanda kwenye soko la dunia.

Mlay alisema kupanda kwa bei ya zao hilo kumechangiwa pia na mahitaji ya bidhaa hiyo duniani kutokana na kuzalishwa katika hali ya ubora ambao unamudu ushindani wa soko la dunia.

Alilipongeza Shirika la Cafe Africa Tanzania, kuwa daraja katika ya wakulima, serikali na wadau kuwasaidia kuinua uchumi wa mkulima mmoja mmoja.



Meneja Programu wa Shirika lisilokuwa la kiserikali la Cafe Africa Tanzania, Samora Mnyaonga (kulia), akitoa elimu kwa wadau na wakulima, kuhusu namna ya kuzalisha zao la kahawa kwa kuzingatia ubora ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi, wakati wa kikao cha kujadili mnyororo wa thamani wa zao hilo kwa mikoa ya Mbeya, Songwe na Ruvuma, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wanaowafanyia ukatili watoto kupewa kibano

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

OFISA Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Songwe, Atusungukye Dzombe, amesisitiza kuwa wataendelea kuwafuatilia na kuwafikisha katika vyombo vya sheria wazazi au walezi wote watakaobainika kuwafanyia vitendo vya ukatili watoto.

Dzombe alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na Nipashe juu ya mikakati ya ofisi yake katika kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyofanyika katika jamii ambapo kwa kiasi kikubwa inawaumiza watoto.

Alisema katika kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia, kesi 640 dhidi ya watoto na wanawake ziliripotiwa mkoani Songwe katika kipindi cha kati ya mwaka 2020/ 2021.

Katika kesi hizo kwa mwaka 2020 kesi za ukatili wa watoto zilizoripotiwa zilikuwa 324, zilizopata mafanikio ni 47, zilizoondolewa na zilikuwa mahakamani ni 117 na kwamba kwa mwaka 2021 kesi zilizoripotiwa ni 316, kati ya hizo zilizofungwa ni 91 zilizopata mafanikio 44 na 134 zinaendelea na upelelezi.

Alisema takwimu hizo zinaonyesha kukithiri kwa vitendo vya ukatili mkoani humo, ili kukomesha wameweka mpango mkakati wa kukabiliana navyo ili kutengeneza kizazi kinachodumisha haki na usawa.

Alisema mkoa umeanza kutoa elimu ya kupinga ukatili na athari zake nyumba kwa nyumba kwa kuwatumia maofisa kuanzia ngazi ya kata ambao wanawafikia ili kuwafundisha namna ya kuondokana na vitendo hivyo pamoja na kukabiliana navyo.

"Aidha, tumeandaa kampeni ya kila wilaya kufanya matamasha ya kuhamasisha wananchi kupinga vitendo vya ukatili kama vile vipigo kwa wanawake, haki ya kumiliki mali, kumsomesha mtoto wa kike na kumpatia mahitaji yake pamoja na mimba na ndoa za utotoni," alisema Dzombe.

Alisema Mkoa wa Songwe bado unakabiliwa na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na kwamba Wilaya ya Mbozi ndio inaongoza kwa vitendo kama vile vipigo na manyanyaso mengine ambavyo huripotiwa katika ofisi yake na Dawati la Jinsia mara kwa mara.

# Waombwa kulinusuru Bonde Ziwa Rukwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MWENYEKITI wa Bonde la Maji Ziwa Rukwa, Herbert Kashililah, amewaomba wadau, wananchi na watumishi kuchukua jitihada za kunusuru bonde hilo na athari za mabadiliko ya tabianchi ambayo yanachangiwa na shughuli za kibinadamu zinafanyika karibu au ndani ya ziwa hilo.

Kashililah alitoa angalizo hilo jana wakati wa kikao cha Jukwaa la nne la wadau wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa, kilichokuwa na lengo la kufanya tathmini ya utekelezaji wa maazimo mbalimbali yaliafikiwa kwenye jukwaa la tatu katika utekelezaji na usimamizi wa bonde hilo.

Alisema jitihada za haraka zinahitajika ili kukabiliana na uvamizi wa shughuli za kinadamu zinazofanywa na baadhi ya wananchi ambao wanajishughulisha na kilimo, uvuvi na ufugaji na kusababisha uharibifu wa mimea na viumbe hai wengine walio ndani ya ziwa hilo.

"Pamoja na kwamba tumekutana kujadiliana utekelezaji wa masuala mbalimbali ya kusimamia Bonde la Ziwa Rukwa, lakini tuliangalie kwa ukaribu suala la uharibifu wa ziwa hilo, madhara yake tunaweza kuyaona hapo baadaye tusipokubali kuchukua hatua za makusudi hivi sasa," alisema Kashililah.

Ofisa Bonde la Maji Ziwa Rukwa, Grace Shitindi, alisema katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Mkoa wa Mbeya walitoa jumla ya miche 340,000 ambayo ilipandwa kwenye vyanzo mbalimbali vya maji ili kulinda uoto wa asili.

Shitindi alisema licha ya kuendelea kupanda miti na mimea ya aina mbalimbali kuendeleza uoto wa asili kuzunguka ziwa hilo vilevile wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira na rasilimali maji.

Mwenyekiti wa Jukwaa la watumia maji mikoa ya Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi, Ulimboka Tuntufye, alisema licha ya kuendelea na shughuli mbalimbali za kujikwamua na uchumi kama vile kilimo, ufugaji, uchimbaji madini na uvuvi lakini bado wanaendelea kusimamia kikamilifu suala la utunzaji mazingira kwa kuzingatia kanuni na sheria za mazingira.

Aliongeza kuwa mara kwa mara wamekuwa wakiandaa midahalo kwa kuwashirikisha wakulima, wafugaji na wachimbaji madini juu ya umuhimu wa kutunza mazingira pamoja na adhabu zinazotolewa kwa yeyote anayebainika kufanya uharibifu wa mazingira.

Naibu Katibu Mkuu kutoka Wizara ya Maji, Dk. Nadhifa Kemikimba, alipongeza kazi kubwa inayofanywa na Bonde la Maji la Ziwa Rukwa katika kuhifadhi rasilimali maji na uoto mwingine wa asili.

Licha ya kutunza mazingira, aliwaomba watumishi kuhakikisha mpango jumuishi wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika bonde la ziwa Rukwa unasimamiwa na kutekelezwa kwa mujibu wa sheria.



# Waagizwa kutumia meli za uvuvi kuongeza upatikanaji samaki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, ameiagiza Taasisi ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) na kampuni ya Hairu iliyoingia ubia wa kuvua samaki, kuzitumia meli za uvuvi na kuhakikisha wanaongeza upatikanaji wa samaki ili kukidhi mahitaji katika soko la ndani.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya boti ya Sehewa 3 kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu kutoka kampuni hiyo ya Sri Lanka amesema hatua hiyo itasaidia wananchi kunufaika na uvuvi wa bahari kuu na serikali kupata mapato.

"Tumewaletea boti hizi ili mtuletee samaki, hivyo ni lazima kwanza mukidhi mahitaji katika soko la ndani na baadaye soko la nje," alisema.

Alisema kwa muda mrefu wananchi walikuwa wakitumia samaki wanaotoka nje ya nchi ambapo baadhi yao walikuwa na hofu juu ya usalama wa samaki hao.

Kuhusu uhaba wa wataalamu wa uvuvi, alisema ana matumaini makubwa kwamba ubia huo utasaidia kuzalisha wataalamu katika sekta hiyo.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema kuja kwa boti hiyo kunaleta matumaini mapya katika sekta ya uvuvi na uwekezaji kutokana na boti hiyo kuwa na zana za kisasa za uvuvi.

Mkurungenzi Uendeshaji wa ZAFICO, Ameir Haidar Msham, alisema boti hiyo ni mahasusi kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu, ambayo inaenda sambamba na utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu.

Alisema ina urefu wa mita 18.5 na uwezo wa kuchukua mabaharia sita, huku ikiwa na uwezo wa kukaa baharini kwa wiki mbili na uwezo wa kuhifadhi samaki zaidi ya tani 18.

Mwenyekiti wa Kampuni ya Hairu, Zainulbdeen Mohamed Hairu, alisema boti hiyo ina huduma zote za mawasiliano na ina nguvu endelevu za kwenda bahari kuu.

**Akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya boti ya Sehewa 3 kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu kutoka kampuni hiyo ya Sri Lanka amesema hatua hiyo itasaidia wananchi kunufaika na uvuvi wa bahari kuu na serikali kupata mapato.**

# Pemba kujenga hospitali ya wagonjwa wa akili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh, amesema serikali inakusudia kujenga hospitali ya magonjwa ya akili kisiwani Pemba baada ya kubainika ongezeko la wagonjwa hao.

Hafidh alisema hayo wakati akijibu hoja za wajumbe waliochangia makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Chukwani.

Alisema wagonjwa wa akili wameongezeka kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo matumizi ya dawa za kulevya kama bangi.

Alizitaja sababu nyengine kuwa ni tatizo la msongo wa mawazo linalotokana na hali ngumu ya maisha.

"Mheshimiwa Spika nakubaliana na michango ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia bajeti hii katika suala la ongezeko la wagonjwa wa akili ambalo linachangiwa na mambo mengi kama matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana na msongo wa mawazo," alisema.

Alisema kwa Unguja huduma kwa wagonjwa wa akili zimeimarika kufuatia kukamilika ujenzi wa jengo la kisasa la kulaza wagonjwa wakiwamo watoto katika mtaa wa Kidongochekundu.

Aliwaomba wananchi kuwapeleka ndugu zao na jamaa wenye matatizo ya akili kupata huduma za kisasa zinazotolewa bure.

Alisema maradhi ya akili yanatibika na kuwataka wananchi kuacha kuyanasibisha na imani za kishirikina.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (kulia), akijadiliana jambo na Mkurugenzi wa Kampuni ya Lab Equip Ltd, Hasan Raza (kushoto) na Meneja Mauzo wa kampuni hiyo, Rehana Mukadam, wakati wa mkutano wa mwaka wa kisayansi ulioandaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), unaoendelea jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Muswada sheria kuimarisha viwanda mbioni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI imesema inakusudia kuwasilisha muswada wa sheria kuimarisha maendeleo ya viwanda Zanzibar ambao miongoni mwa majukumu yake ni kulinda viwanda na kuhakikisha vinachangia pato la taifa na kutoa ajira kwa vijana.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, wakati akitoa ufafanuzi kuhusu mikakati ya serikali ya kulinda viwanda vyake ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa vipaumbele vya serikali kuzalisha ajira 300,000 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema mikakati ya serikali ya awamu ya nane ni kuhamasisha wawekezaji zaidi kuwekeza katika miradi ya ujenzi wa viwanda ambavyo vitasaidia kuzalisha ajira kwa wananchi.

"Mheshimiwa Spika serikali imejipanga kuleta muswada ambao utalinda viwanda vyetu kwa kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji hatua ambayo itaongeza mapato na kukuza uchumi," alisema.

Alisema tayari serikali imefanikiwa kutenga maeneo matatu kwa ajili ya wawekezaji katika sekta ya viwanda ikiwamo Dunga Wilaya ya Kati, Pangatupu Donge na Chamanangwe Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Kadhalika, tayari maeneo hayo yamepatiwa hatimiliki ili kuepuka uvamizi unaofanywa na watu kwa kujenga makazi ya kudumu.

Hata hivyo, alisema maeneo huru ya uchumi ya Micheweni Pemba na Fumba Unguja yanaendelea kutumiwa na wawekezaji.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe**

**Kituo cha Njombe mjini**
**Mkoa wa Njombe.**

**Usimamizi wa mirathi na 63/2021.**

**Benard Lupyana Mgina ::::::::::::::Marehemu.**
**Paulina Samweli Mbaha:::::::::::: Msimamizi**

### TAARIFA KWA UMMA
**MAOMBI YA KUFUNGA MIRATHI**

Kwa wote wanaodai kuwa na haki na Marehemu aliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya Mali za Marehemu na hesabu za mirathi katika jalada la mirathi.

Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya Mali na au hesabu za mirathi hii yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya siku ya tarehe 27 ya mwezi wa mei mwaka 2022

Imetolewa na Hakimu mkazi leo siku ya tarehe 27 April mwaka 2022.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA)**
**Mahakama ya mwanzo ya ARUSHA MJINI wilaya ya ARUSHA**
**MIRATHI –MADAI NAMBARI 238 YA 2016**
**Muombaji BETTY ISACK MASALA**
**Amdai**
**Mdaiwa BETTY ISACK MASALA**

**Kwa, BETTY ISACK MASALA WA DAR ES SALAAM**
**Kwa kuwa mdai/mdaiwa ameleta/wameleta madai yake/yao**

Unaamriwa kufika mahakamani bila kukosa kuja kujibu madai ya mirathi yanayokukabili

Kwahiyo unahitajika /mnahitajika kufika kuhudhuria mahakama hii siku ya jumanne tarehe 24/05/2022 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwakuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zinazohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo

Kama hukuhudhuria /hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikithibitika kama umepokea /mmepokea kuitwa shauri hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 25/04/2022

---

## KUPOTEA KWA CHETI/RESULT SLIP



**ABDIRAHAMANI HAFIDHI KIZUA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0783/0039** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia BEREKO SEKONDARI mwaka 2016 pamoja na Result Slip. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/MUR/RB/190808/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mhakama ya mwanzo ya wilaya ya Temeke**

**Kituo cha Jumuishi Mkoa Dar es salaam**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 758/ 2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SAIDI OMARY MSATI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA PILI SAIDI NGUVUZE**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 Mwezi wa 5 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 19 Mwezi wa 04 Mwaka 2022.

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya**
**Wilaya ya Morogoro**
**Kituo cha Kingolwira**
**Mkoa Wa Morogoro**
**Shauri la Mdai na.17/2022**
**Jina la mdai YASSIRI MOHAMED SIMBA**
**Jina la Mdaiwa LEONARD SHIMBA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: LEONARD SHIMBA KAHAMA**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta madai yake /yao kwamba**:MADAI YA PESA SHS.20,000,000.**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe **26/05/2022 saa 8:30 asubuhi** kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kijitetea.

**ANGALIZO:**kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 17/05/2022.

**HAKIMU**

---


## Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

## Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Mazungumzo kumaliza vita yavunjika, Ukraine, Russia zavutana kuhusu mateka

**KYIV,** UKRAINE

HATIMAYE Russia na Ukraine zimesitisha mazungumzo ya kumaliza vita baada ya kuzuka hali ya kutoaminiana kwa pande zote.

Hata hivyo, mzozo mwingine umeibuka kuhusu uwezekano wa kubadilishana wafungwa katika mji uliozingirwa wa Mariupol.

Jumla ya wanajeshi 265 wa Ukraine walijisalimisha kwa mamlaka ya Russia.

Kiongozi wa ujumbe wa Ukraine Mykhailo Podolyak, alisema hatua zisingepigwa katika mazungumzo hayo kama Russia haitaki kuitambua hali ilivyo kwenye uwanja wa mapambano.

Alisema madai ya Russia kuwa inapambana na Unazi nchini humo hayana msingi wowote.

Aliongeza kwamba mpango wa kusitishwa mapigano unaweza kujadiliwa kama wanajeshi wote wa Russia wataondoka nchini humo na maeneo yote yaliyotekwa.

Naibu Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Russia, Andrei Rudenko, alisema mazungumzo hayo hayatoendelea kwa sababu Ukraine imejiondoa.

Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz, alizungumza jana kwa njia ya simu na Rais Volodymyr Zelensky na kukubaliana kuwa suluhisho la mazungumzo ya kidiplomasia kati ya Ukraine na Russia ni muhimu ili kumaliza vita hivyo.

**WANAJESHI 959 WA UKRAINE WAMEJISALIMISHA**

Wizara ya Ulinzi ya Russia ilisema zaidi ya wanajeshi 900 wa Ukraine, wamejisalimisha wiki hii katika kiwanda cha chuma cha Azovstal mjini Mariupol.

Katika taarifa yake ya kila siku kuhusiana na mzozo huo, wizara hiyo ilisema jumla ya wanajeshi 959 wamejisalimisha tangu Mei 16, na 80 kati yao wakiwa majeruhi.

Wizara hiyo ilisema wale wanaohitaji matibabu wamepelekwa katika hospitali moja iliyoko mji wa Novoazovsk unaodhibitiwa na Russia.

Ukraine inatarajia kuwabadilisha wafungwa wa Russia na wanajeshi hao waliojisalimisha ila Russia haijathibitisha iwapo hilo litafanyika.

Mwezi uliopita, Russia ilidai kuchukua udhibiti wa Mariupol baada ya wiki kadhaa za mashambulizi, ila mamia ya wanajeshi wa Ukraine walikuwa wamejificha katika mahandaki ya chini ya ardhi kwenye kiwanda hicho cha Azovstal.

Wizara ya ulinzi ya Ukraine ilisema itafanya kila iwezalo kuwanusuru wapiganaji waliosalia kiwandani humo ambao idadi yao haijulikani hadi sasa, ila ilidai hawatofanya operesheni ya kijeshi.

**SWEDEN NA FINLAND ZAWASILISHA MAOMBI NATO**

Mabalozi wa Sweden na Finland wamewasilisha rasmi jana maombi yao ya kujiunga na Jumuiya ya Kujihami ya NATO kwa Katibu wake Mkuu Jens Stoltenberg.

Hayo yalifanyika katika hafla ya video mjini Brussels. Wakati akipokea maombi hayo, Stoltenberg alisema hatua hiyo ni ya kihistoria katika wakati muhimu kwa usalama wa Ulaya.

"Wanachama wa NATO sasa watazingatia hatua zinazofuata kuelekea nchi zenu kuwa wanachama. Usalama wa wanachama wote lazima uzingatiwe pia katika mchakato huu na tunadhamiria kuangazia masuala yote na tupate suluhisho la haraka." Alisema.

Nchi hizo zilianza mchakato wa kutaka kujiunga na muungano huo wa kijeshi kutokana na uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

Russia ilisema maombi hayo ya Sweden na Finland kutaka kuwa wanachama wa NATO hayaleti tofauti yoyote kwa kuwa nchi hizo zimekuwa zikishiriki luteka za kijeshi na muungano huo wa kujihami.

ICC yatuma wapelelezi Ukraine

Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Kivita (ICC) imeituma timu ya maofisa 42 nchini Ukraine kuchunguza tuhuma za uhalifu wa kivita tangu Russia ilipovamia Februari 24 mwaka huu.

Mahakama hiyo ilisema kikosi hicho ni kikubwa cha maofisa kuwahi kutumwa katika historia yake.

Mwendesha mashitaka mkuu wa ICC Karim Khan amesema timu hiyo itahakikisha kuwa ushahidi unakusanywa katika njia ambayo inaweza kusaidia kutumiwa mahakamani katika siku za usoni.

Timu hiyo inajumuisha wapelelezi, wataalamu wa kukusanya ushahidi na maofisa wasaidizi na watashirikiana na mamlaka za Ukraine.

ICC ilitangaza kuanzisha uchunguzi kuhusu madai ya uhalifu wa kivita dhidi ya ubinadamu siku nne tu baada ya uvamizi. **DW**



Baadhi ya wanajeshi wa Ukraine waliookolewa ndani ya kiwanda cha chuma katika mji wa Mariupol wakiwa ndani ya basi wakielekea katika mji unaomilikiwa na waasi. **PICHA: DW**

## Raila Odinga aongoza kwa umaarufu Kenya

**NAIROBI,** KENYA

UMAARUFU wa kiongozi wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga, umeongezeka kwa asilimia tatu na kufikia asilimia 39 dhidi ya mpinzani wake mkuu naibu rais wa taifa hilo, William Ruto.

Kulingana na utafiti uliofanywa na shirika la TIFA, Ruto umaarufu wake umepungua kutoka asilimia 39 na kufikia asilimia 35.

Utafiti huo unaonyesha Odinga amepanda kutokana na hatua yake kumteua mgombea mwenza mwanamke, ambaye alikuwa waziri wa haki Martha Karua.

Jumla ya raia 1, 719 wa Kenya walishiriki katika tafiti hiyo ambapo walihojiwa kupitia njia ya simu.

Odinga ambaye aliwahi kuhudumu kama waziri mkuu nchini Kenya, katika kura ya maoni ya mwezi Aprili, alikuwa na asilimia 32 ya umaarufu dhidi ya Ruto aliyekuwa na asilimia 38.

TIFA katika utafiti wao pia wamebaini kuwa chama cha naibu rais Ruto, UDA, kinaongoza kwa umaarufu kwa asimilia 29 dhidi ya kile cha Odinga kwa asilimia 25.

Uchaguzi wa urais nchini Kenya, unatarajiwa kufanyika Agosti 9 mwaka huu, kipindi cha kampeni kikitarajiwa kuanza mwisho wa mwezi huu.

**RFI**

## Somalia yawakaribisha wanajeshi wa Marekani

**MOGADISHU,** SOMALIA

RAIS mpya wa Somalia, Hassan Shekhe Mohamud, amekaribisha mpango wa Marekani kurejesha wanajeshi wake nchini humo, kusaidia serikali kupambana na magaidi wa Al- Shabab.

Kupitia taarifa kwa mtandao wake wa Twitter, Rais Mohamud, alisema Marekani imekuwa mshirika wake wa karibu katika vita dhidi ya ugaidi.

Utawala wa Biden, wiki hii ulitangaza mpango wa kuwatuma zaidi ya wanajeshi 600 nchini Somalia, kukabiliana na wapiganaji wa al-Shabab.

Hatua hiyo ya Marekani ilichukuliwa siku moja baada ya wabunge wa nchi hiyo, kumteua Rais Mohamud, kuhudumu kwa mara nyingine katika uchaguzi ambao ulikuwa umecheleweshwa, kutokana na mgogoro wa kisiasa.

Wapiganaji wa al-Shabaab hawajatoa taarifa yoyote kuhusiana na hatua hiyo ya Marekani.

**RFI**

# MPOLE AANIKA NDOTO ZA ULAYA AKIMFUNIKA MAYELE MBIO KIATU

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI akizidi kukimbiza kwenye mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu Bara, straika wa Geita Gold FC, George Mpole, amesema malengo yake ya muda mrefu ambayo anaendelea kuyapigania kila uchao ni kucheza soka la kulipwa Ulaya.

Mpole ambaye kwa sasa yupo kileleni mwa orodha ya wafungaji bora Ligi Kuu Bara akiwa na mabao 13, baada ya juzi kuifungia timu yake bao pekee wakati ikiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Mbeya Kwanza katika Uwanja wa Majimaji mkoani Songea, ameisaidia Geita Gold kukwea hadi nafasi ya nne ikiwa na alama 34 baada ya kushuka dimbani mara 24.

Akizungumza na mwandishi wetu juzi, Mpole alisema lengo lao kubwa ni kumaliza wakiwa kwenye nafasi ya tatu au ya nne, huku ufungaji bora ikiwa ni lengo la pili, lakini ndoto yake kubwa ni kuendelea kuonyesha uwezo uwanjani ili kupata timu Ulaya.

"Malengo yangu ni kucheza soka la kulipwa Ulaya, hiyo ni ndoto ambayo ninayo muda mrefu, ninaamini zitatimia, kamwe sitakata tamaa hadi nifanikiwe," alisema Mpole ambaye sasa anampita mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele kwa bao moja.

Alisema licha ya msimu huu kuwa na ushindani kwa upande wake, atapambana kuhakikisha anabeba Kiatu cha Ufungaji bora.

"Malengo yangu msimu huu ni kuwa mfungaji bora pamoja na kuifikisha mahali pazuri timu yangu nikishirikiana na wachezaji wenzangu," alisema.

Alisema anaomba Mungu washike nafasi ya juu kwenye msimamo wa ligi hiyo, kwani anaamini bila kumtanguliza Mungu asingefika alipo sasa.

"Mafanikio yote yanatokana na mipango ya Mungu, ambaye yeye ndiye muweza wa kila jambo, ninaomba mashabiki wangu waendelee kuniamini nitapambana kadri niwezavyo," alisema.

# Julio achekelea pointi sita siku moja

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Namungo FC, Jamhuri Kihwelo 'Julio', ameonyesha kufurahishwa na timu yake kupata pointi sita kwa siku moja, wakati ikiichapa Biashara United mabao 2-1 juzi kwenye Uwanja wa Nyamagana Mwanza, huku uamuzi wa kupewa pointi tatu na mabao matatu na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), ukitolewa kutokana na Mbeya Kwanza kugomea mechi.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kumalizika, alisema yeye, wachezaji wake na viongozi wamefurahi kupata pointi tatu ugenini dhidi ya Biashara United kwa sababu wamezitolea jasho uwanjani, huku wakitoka safari ya mbali mkoani Lindi hadi Mwanza kwa ajili ya kuzisaka.

"Tunashukuru Mungu, tumetoka safari ya mbali sana, kutoka Lindi hadi Mwanza, tukapata pointi tatu ni jambo la kushukuru na kujisikia faraja," alisema.

Yalikuwa ni mabao ya Shiza Kichuya dakika ya nane na 67, yakiiwezesha timu hiyo kupata ushindi huo, huku la kufutia machozi la Biashara United inayotumia uwanja huo, likifungwa na Ambrose Awio.

Wakati wakipata pointi hizo tatu, Namungo ikaongezewa pointi zingine kama hizo juzi baada ya Kamati ya TPLB kuipa ushindi kutokana na Mbeya Kwanza kugomea mchezo kwa madai ya kutokuwapo kwa gari la wagonjwa uwanjani na hata lilipokuja, muda wa kikanuni ulikuwa umepita.

Kamati ilidai baada ya kupokea taarifa, ilifanya uchunguzi na kubaini gari hilo lenye namba STL 3096 lilifika uwanjani hapo, lakini liliondoka kwa dharura kabla ya muda wa mchezo.

Ikasema waandaaji wa mchezo, Chama cha Soka Lindi kwa kushirikiana na kamisaa wa mchezo walikubaliana kutafuta gari linaloweza kutumika kubeba majeruhi kabla gari hilo maalum halijarejea, lakini Mbeya Kwanza walipinga, pamoja na gari hilo kurejea kabla ya muda.




Shiza Kichuya (jezi namba 25), akishangilia baada ya kuifungia timu yake moja kati ya mabao mawili aliyotupia wakati wakishinda 2-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Biashara United katika Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza juzi. **PICHA: NAMUNGO**

Julio alisema walistahili kupata pointi hizo, na pia alitegemea kwa sababu wenzao hawakutaka kucheza mpira, ila kutafuta pointi za mezani.

"Wachezaji wao walitaka kucheza, lakini baadhi ya viongozi hao wakapinga kabisa, wakagomea, tuliathirika kwa sababu tuliingia gharama ya kujiandaa na mchezo huo, hivyo tumestahili," alisema.

Kwa matokeo hayo, Namungo imefikisha pointi 36, ikiwa kwenye nafasi ya tatu ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

## KMC FC, Mbeya City zatambiana

**Na Saada Akida**

MAKOCHA wa Timu ya KMC FC na Mbeya City, kila mmoja ametamba kuhitaji pointi tatu wakati timu hizo zitakaposhuka dimbani katika mechi ya Ligi Kuu itakayopigwa leo katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam majira saa 10:00 alasiri.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana, Kocha Msaidizi wa KMC FC, Ahmad Ally, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanafanikiwa kuzuia alama tatu katika uwanja wa nyumbani.

Alisema hawana majeruhi na wachezaji wote wako vizuri na tayari kwa ajili ya mchezo huo kuhakikisha wanatafuta ushindi katika mechi hiyo.

"Hii ni mechi ngumu na ushindani mkubwa kwa sababu ukiangalia tunaenda kukutana na timu ambayo iko nafasi ya sita, tukishinda mechi tunamsogelea na kupanda hadi nafasi ya saba," alisema Ahmad Ally.

Kocha Msaidizi wa Mbeya City, Antony Mwamlima, alisema wamejiandaa vizuri na watashuka dimbani kwa nidhamu ya hali ya juu kuhakikisha wanapata matokeo mazuri ya kuvuna alama tatu.

"Hali ya hewa ya Mbeya ni Baridi na Dar es Salaam ni joto, lakini haitatuathiri mipango yetu kwa sababu tumejiandaa katika kuhakikisha tunarudi nyumbani na pointi muhimu ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kufikia malengo yetu ya kuwania nafasi ya nne," alisema Mwamlima.

## Mgunda atangaza tatu za kufa kupona

**Na Cheji Bakari, Tanga**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, ametangaza mechi tatu za kucheza kufa kupona ili kuibuka na ushindi, mbili kati ya hizo zikiwa ni za Ligi Kuu na moja ya Kombe la Shirikisho nchini, maarufu Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC).

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Mgunda alizitaja mechi hizo kuwa ni dhidi ya Dodoma Jiji mchezo utakaochezwa katika Uwanja wa Mkwakwani Mei 20 na baada ya hapo kwenda jijini Mbeya kuvaana na Mbeya City katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine.

Mgunda alisema baada ya mchezo huo watasafiri kuelekea jijini Arusha tayari kwa mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Azam FC itakayopigwa Mei 28, mwaka huu, katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid.

"Tuna mechi tatu muhimu dhidi ya Dodoma Jiji FC, Mbeya City na ule wa Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) dhidi ya Azam FC na michezo yote ni muhimu tunatakiwa tushinde, kikosi changu kipo vizuri, tuombe Mungu," alisema Mgunda.

## ZISIKUPITE

### JESUS LULU ARSENAL
ARSENAL wanamtaka mshambuliaji mwenye umri wa miaka 25, Gabriel Jesus ambaye ameripotiwa kuwa tayari kumpa mshahara mkubwa. ***(Telegraph)***

### WEIR KUTUA MADRID
KIUNGO wa kati wa Manchester City, Caroline Weir mwenye umri wa miaka 26, anakaribia kuhamia Real Madrid kwa uhamisho huru msimu huu. ***(Telegraph)***

### UMTITI KUONDOKA BARCA
BARCELONA wameamua kumuacha mlinzi wao, Samuel Umtiti aondoke mwishoni mwa msimu huu, huku wakiwa na matumaini kuwa kocha wa Arsenal, Mikel Arteta atamtaka nyota huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Star)***

### BARCA NA LEWANDOWSKI
BARCELONA wako tayari kuweka bajeti ya euro milioni 35 ili kumsajili mshambuliaji wa Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33, kutoka Klabu ya Bayern Munich na inaweza kumtoa mshambuliaji wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 28, Memphis Depay kama sehemu ya mkataba huo. ***(Mundo Deportivo)***

### MESSI KWENDA MAREKANI
MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 34, atajiunga na Ligi ya Kuu ya Marekani katika klabu ya Inter Miami mwaka 2023, wakati mkataba wake wa miaka miwili kule Paris St-Germain utakapomalizika. ***(Direct TV, via Marca)***

### POGBA NA OFA JUVE
JUVENTUS wamempatia ofa kiungo wa kati Mfaransa Paul Pogba, ambaye atakuwa tayari kwa uhamisho huru wakati mkataba wake na Manchester United utakapofika ukingoni mwishoni mwa msimu huu. ***(Goal)***

### BOTMAN KUTUA UNITED
KLABU ya Manchester United imewasiliana na nyota wa Lille, Sven Botman huku wakijaribu kuipiku AC Milan kusaini mkataba na mchezaji huyo wa mwenye umri wa miaka 22 . ***(Football Insider)***

### DE LIGT KUJIFUNGA TENA
MLINZI wa kati wa Uholanzi, Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 22, anakaribia kusaini mkataba mpya utakaomuwezesha kucheza katika kikosi cha Juventus hadi mwaka 2026 . ***(Sky Sport Italia, via 90 Min)***

### DI MARIA AIKUBALIA JUVE
WINGA wa Argentina, Angel di Maria mwenye umri wa miaka 34, amekubali mkataba wa mwaka mmoja na Juventus na atajiunga na klabu hiyo ya Serie A wakati mkataba wake na Paris St-Germain utakapomalizika msimu huu.***(Goal)***

### TIMBER ATAJWA UNITED
MLINZI wa Ajax, Jurrien Timber mwenye umri wa miaka 20, pia analengwa na Manchester United. ***(Mirror)***

### DENNIS ANUKIA WEST HAM
KLABU ya West Ham ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Nigeria mwenye umri wa miaka 24, Emmanuel Dennis kutoka Watford. ***(Mirror)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA YATAJA SABABU KUMPOTEZEA MBAPPE

●●●Laporta aanika kila kitu, ni wakati Real Madrid na PSG zikiendelea kupigana vikumbo...

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Klabu ya Barcelona, Joan Laporta, ameweka wazi kiasi cha mshahara ambao nyota wa Klabu ya Paris Saint Germain, Kylian Mbappe alichohitaji wakati akifanyiwa mahojiano na Cat Radio.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye miaka 23, yupo kwenye mwezi wake wa mwiasho na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, huku bado kukiwa na kitendawili cha wapi atacheza kwa msimu ujao.

Real Madrid ndio klabu iliyohusishwa naye sana kuliko klabu yoyote ile, lakini uhamisho huo unaonekana hautafanyika kipindi hiki.

Laporta aliweka wazi kiasi ambacho walipewa ikiwa watahitaji huduma ya mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2018.

kwa mujibu wa Laporta, Mbappe alihitaji kiasi cha euro milioni 50 kama mshahara wake kwa mwaka, kitu ambacho kisingewezekana kutokana na matatizo ya kifedha ambayo klabu hiyo ilikuwa nayo.

"Kylian Mbappe alihitaji kiasi cha euro milioni 50 kwa mwaka," alisema Laporta

Kwa sasa Mbappe bado haijajulikana ni wapi atamwaga wino kwa msimu ujao, huku kukiwa na taarifa mbili za kila upande, PSG wanadai kuwa wana uhakika wa kumbakisha na Real Madrid nao wanadai kuwa tayari washafanya mazungumzo ya awali.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 200,

MECHI KALI
EVERTON
VERSUS
CRYSTAL PALACE
1 | 1.83
X | 3.47
2 | 4.06

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SKRTEL ASTAAFU KUCHEZA SOKA




**LIVERPOOL, England**

NYOTA wa zamani wa klabu ya Liverpool, Martin Skrtel, ameamua kutundika daluga akiwa na miaka 37, huku sababu kubwa ya kuachana na soka ikiwa ni matatizo ya kiafya baada ya kucheza soka kwa miaka 21.

Skrtel aliichezea klabu ya Liverpool kwa miaka nane pia alikuwa mchezaji muhimu chini ya Rafael Benitez kwenye msimu wa 2008/09 na Brendan Rodgers kwenye msimu 2013/14 katika mbio za kutafuta ubingwa ambao hawakufanikiwa na walishika nafasi ya pili.

Skrtel akizungumza kwa uchungu kwenye kikao na waandishi wa habari alisema, "kurudi Trnava, nilitimiza ndoto yangu, nafikiri kwamba hata katika umri huu bado kuna kitu naweza kuchangia kwenye timu na kuweza kucheza katika uwezo wangu wa juu.

"Lakini kuna tatizo la kiafya linanizuia si tu kwenye soka, lakini pia kwenye maisha yangu ya kawaida. Sikumbuki siku ambayo imekwisha pasipo maumivu.

"Nimekuwa na tatizo la kutembea umbali wa mita mia na mwanangu. Maumivu ni makali sana, mbaya zaidi nikikimbia, kuruka na hili ndilo tunalohitaji kwenye soka."

Skrtel mchezaji wa kimataifa wa Slovakia ameichezea Liverpool michezo 320 kwa muda wake wote aliokaa kwenye klabu hiyo.

# Di Maria kutimkia Juve kwa uhamisho huru

**PARIS, Ufaransa**

MCHEZAJI wa kimataifa wa Argentina, Angel Di Maria anajiandaa kuondoka katika klabu ya Paris Saint-Germain na kujiunga na Juventus kwa uhamisho huru, hii ni kwa mujibu wa vyanzo vya habari za soka nchini Italia.

Nyota huyo ambaye ameitumikia PSG kwa miaka saba sasa, yupo kwenye mwaka wake wa mwisho katika mkataba wake ambao unatarajiwa kufikia kikomo mwishoni mwa msimu huu wa 2021-22.

Juve wamekuwa wakihusishwa na kutaka kumnunua Di Maria na kwa mujibu wa Football Italia, imeeleza kuwa dili hilo lipo karibu kukamilika.

Di Maria atapokea mkataba wa mwaka mmoja na chaguo la miezi 12 zaidi na mshahara wa euro milioni saba kwa mwaka.

Di Maria alijiunga na PSG akitokea Man United mwaka 2015, lakini kabla ya kujiunga na 'Mashetani Wekundu' hao, alitumia misimu minne akiwa na Real Madrid na kufanikiwa kutwaa mataji ya LaLiga, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Copa del Rey (Kombe la Mfalme).



,000,000




Mshindi wa Jackpot ya SportPesa ya Sh. 1,255,316,060, Florian Valerian Massawe akionyesha mfano wa hundi baada ya hafla ya kukabidhiwa rasmi na SportPesa jana. **PICHA: SPORTPESA**

# MASSAWE WA KILUVYA WA BILIONI 1.2/- ZA SPORTPESA HUYU HAPA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Michezo na Burudani ya SportPesa imemtambulisha rasmi mshindi wa Jackpot ya shilingi 1,255,316,060, Florian Valerian Massawe (36), kutoka Kiluvya, Dar es Salaam.

Florian ambaye ni fundi makenika amefanikiwa kuwa bilionea wa kwanza wa SportPesa baada ya kubashiri kwa usahihi mechi zote 13 za Jackpot za wiki iliyopita.

Akimtambulisha mshindi huyo wa awamu ya nane mbele ya waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas, alianza kwa kumpongeza Florian kwa ushindi wake na kuwa bilionea wa kwanza aliyetokana na kubashiri mpira wa miguu.

"Leo ni siku ya furaha kwangu na kwa wafanyakazi wengine wote wa SportPesa kwa kumpata mshindi wa Jackpot. Napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya kampuni kumtambulisha kwenu Florian Valerian Massawe kuwa mshindi rasmi wa Jackpot yetu akiwa amejishindia zaidi ya bilioni 1.2," alisema Tarimba.

"Kwa bahati nzuri mshindi wetu amepatikana wakati tunasherehekea miaka mitano tangu kuanza shughuli hizi za michezo ya kubashiri hapa Tanzania. Ushindi wa Florian umefanikisha dhamira yetu ya kuwawezesha na kuwainua Watanzania kiuchumi na kutengeneza bilionea wa kwanza.

"Nyote ni mashahidi leo kiwango hiki cha pesa alichoshinda ni kikubwa na kitainua maisha yake na familia yake na pia jamii ambayo anaishi nayo.

"Hili ni jambo la kihistoria kwa kampuni yetu kuwa ya kwanza kumtangaza mshindi wa kiasi kikubwa (bilioni 1.2) kwenye sekta ya michezo ya kubashiri ambaye leo anakabidhiwa hundi ya pesa aliyoshinda."

Akizungumza kwa niaba ya TRA Mkuu wa kitengo cha michezo ya kubahatisha, Shabani Mwanga alimpongeza kwa ushindi alioupata wa zaidi ya bilioni moja na pia kama Mtanzania mzalendo, amechangia kwenye uchumi wa nchi kwa kodi ambayo imetokana na ushindi wake wa Jackpot.

"Kama mwakilishi wa TRA, nimefarijika kwa ushindi wako na pia kwa mchango ambao umeutoa si kwa kiwango hiki tu cha bilioni 1.2 tu, bali hata kwa siku za nyuma ambazo umekuwa ukicheza na ukishinda.

"Kwa ushindi huu Florian amechangia jumla ya shilingi 188,297,109 kama kodi, ikiwa ni asilimia 15 ya makato katika pesa aliyoshinda ya shilingi 1,255,316,060 na hivyo atabakiwa na shilingi 1,067,018,951 kama faida yake," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), James Mbalwe, alimpongeza Florian kwa ushindi na kumtaka kuendelea kuwa mwadilifu kwani pesa aliyoshinda ni nyingi hivyo zinaweza kumfanya akageuka.

"Nachukua nafasi hii kukupongeza kama ambavyo wenzangu waliotangulia walivyofanya na pia napenda kuwaasa Watanzania kuamini bodi ya michezo ya kubahatisha.

"Kwa umri bado wewe ni kijana na hii pesa uliyoshinda ni nyingi, tungependa uwe mfano mwema kwa wengine kwa kufanya yale yenye manufaa kwako na kwa familia yako.

Akitoa neno la shukrani kwa SportPesa, Florian alisema kwanza kwake imekuwa ndoto ambayo imetimia katika muda mfupi kwani alianza kucheza bila kukata tamaa tangu mwaka 2017.

"Najua wengi mnaweza msiamini, lakini mimi nilikuwa nacheza karibu kila wikiendi kuanzia mikeka 2 mpaka 5 nikiamini ipo siku nitafanikiwa, Mungu mkubwa leo (jana), nipo mbele yenu natambulishwa kama mshindi wa Jackpot kubwa kabisa ya baba lao ya Sportpesa ya shilingi 1,255,316,060," alisema.

"Pesa hii inakwenda kubadili maisha yangu kabisa na namuomba Mwenyezi Mungu aniongoze ili niweze kuizalisha zaidi na zaidi."


JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/05/22 | 18:00 | Crystal Palace vs Manchester Utd | 2.89 | 3.32 | 2.31 |
| 02. 22/05/22 | 18:00 | Brentford vs Leeds | 2.28 | 3.42 | 2.87 |
| 03. 22/05/22 | 18:00 | Burnley vs Newcastle | 2.34 | 3.22 | 2.92 |
| 04. 22/05/22 | 18:00 | Brighton vs West Ham | 2.45 | 3.30 | 2.71 |
| 05. 22/05/22 | 18:00 | Brondby vs Silkeborg | 2.48 | 3.59 | 2.54 |
| 06. 22/05/22 | 18:30 | Kalmar vs Djurgardens IF | 2.77 | 2.97 | 2.48 |
| 07. 22/05/22 | 18:30 | Elche vs Getafe | 3.05 | 2.95 | 2.49 |
| 08. 22/05/22 | 19:00 | Stromsgodset vs Valerenga | 2.64 | 3.29 | 2.54 |
| 09. 22/05/22 | 19:00 | Jerv vs Odd Ballklubb | 2.90 | 3.25 | 2.37 |
| 10. 22/05/22 | 21:00 | Ham-Kam vs Rosenborg | 2.53 | 3.27 | 2.68 |
| 11. 22/05/22 | 23:00 | Real Sociedad vs Atletico Madrid | 2.65 | 3.25 | 2.60 |
| 12. 22/05/22 | 23:00 | Barcelona vs Villarreal | 2.47 | 3.60 | 2.58 |
| 13. 22/05/22 | 23:00 | Sevilla FC vs Athletic Bilbao | 2.35 | 3.35 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 19/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1641 | Sagamihara vs Yokohama SCC | 1.75 | 3.40 | 4.27 |
| 16:00 | 5580 | KMC vs Mbeya City | 2.37 | 2.67 | 3.30 |
| 17:00 | 1710 | CA 3 De Febrero vs Club Guarani De Trinidad | 2.30 | 2.87 | 3.16 |
| 17:00 | 5989 | Radnik Surduluca vs Kolubara | 2.22 | 3.21 | 2.97 |
| 17:15 | 2047 | Maccabi Kishronot Hadera W vs Bnot Netanya W | 1.25 | 5.82 | 7.76 |
| 17:30 | 2320 | Teraktor Sazi vs Persepolis FC | 5.65 | 2.92 | 1.72 |
| 18:00 | 1004 | MKS Kutno vs Unia Skierniewice | 2.77 | 3.35 | 2.27 |
| 18:00 | 2018 | US Ben Guerdane vs Esperance Tunis | 9.35 | 3.46 | 1.42 |
| 18:00 | 3105 | Harju JK Laagri vs Paide Linnameeskond | 2.27 | 4.49 | 2.45 |
| 18:00 | 3786 | FK Liepaja vs FS Metta/Lu | 1.07 | 8.37 | 21.42 |
| 18:00 | 3899 | VPS Vaasa vs Inter Turku | 3.35 | 3.26 | 2.02 |
| 18:30 | 1346 | Peykan FC vs Foolad Khuzestan | 3.65 | 2.55 | 2.48 |
| 18:30 | 3947 | Gol Gohar vs Naft Masjed Soleyman FC | 1.48 | 3.46 | 7.40 |
| 18:30 | 4430 | Sepahan Esfahan vs Padideh Mashhad | 1.33 | 4.60 | 10.00 |
| 18:30 | 4515 | Fajr Sepasi vs Zob Ahan | 3.55 | 2.48 | 2.41 |
| 19:00 | 1214 | Rana FK vs Bodo Glimt | 34.09 | 18.50 | 1.01 |
| 19:00 | 1340 | Byaasen Toppfotball vs Kolstad | 1.49 | 4.65 | 4.65 |
| 19:00 | 2043 | Melhus vs Strindheim IL | 3.80 | 4.58 | 1.62 |
| 19:00 | 2216 | Viimsi JK-Ida vs Virumaa FC Alliance | 1.25 | 6.00 | 9.61 |
| 19:00 | 3206 | Flora II vs FC Elva | 1.74 | 4.21 | 3.86 |
| 19:00 | 3806 | Kolbu/KK vs Valerenga | 28.29 | 12.68 | 1.01 |
| 19:00 | 4287 | Verdal vs Rosenborg | 29.09 | 15.52 | 1.01 |
| 19:00 | 4813 | FCI Levadia Tallinn U21 vs Viljandi Tulevik | 1.07 | 11.01 | 22.02 |
| 19:00 | 5037 | Honefoss vs Stromsgodset | 28.29 | 12.68 | 1.01 |
| 19:00 | 5072 | Tiller IL vs Nardo | 3.12 | 4.39 | 1.81 |
| 19:00 | 5448 | Dahle IL vs Ranheim | 14.58 | 7.77 | 1.11 |
| 19:30 | 1188 | Sanat Naft Abadan vs MES Rafsanjan | 3.07 | 2.49 | 2.68 |
| 19:30 | 2239 | Hobro vs Vendsyssel FF | 2.23 | 3.25 | 2.91 |
| 19:30 | 5595 | HB Koge vs Jammerbugt FC | 1.41 | 4.37 | 6.21 |
| 19:45 | 3477 | Heerenveen vs AZ Alkmaar | 3.56 | 3.66 | 1.90 |
| 19:45 | 3517 | Esteghlal Tehran vs Aluminium Arak | 1.54 | 3.16 | 7.38 |
| 20:00 | 2187 | Brommapojkarna vs Ostersunds | 1.53 | 4.35 | 5.67 |
| 20:00 | 2584 | FC Sarajevo vs Velez Mostar | 2.53 | 3.07 | 2.63 |
| 20:00 | 2713 | IK Brage vs Dalkurd FF | 1.65 | 3.94 | 5.05 |
| 20:00 | 4240 | Rigas Futbola Skola vs FK Tukums 2000/Tss | 1.04 | 12.00 | 40.00 |
| 20:00 | 4943 | AFC Eskilstuna vs Norrby IF | 2.53 | 3.50 | 2.64 |
| 20:00 | 5640 | Osters IF vs Halmstads BK | 2.74 | 3.25 | 2.59 |
| 20:30 | 1165 | Sepsi Osk vs Voluntari | 2.15 | 2.97 | 3.36 |
| 21:30 | 2061 | Lausanne vs Sport-FC Sion | 2.73 | 3.58 | 2.33 |
| 21:30 | 2531 | Servette Geneva vs FC Basel | 3.15 | 3.75 | 2.04 |
| 21:30 | 2630 | FC Lugano vs FC Zurich | 2.48 | 3.52 | 2.58 |
| 21:30 | 2800 | Hertha BSC vs Hamburger SV | 2.29 | 3.26 | 2.97 |
| 21:30 | 3522 | Grasshoppers vs St. Gallen | 2.02 | 3.68 | 3.24 |
| 21:30 | 4540 | FC Luzern vs BSC Young Boys | 3.98 | 4.08 | 1.73 |
| 21:45 | 1148 | Port Vale vs Swindon Town | 2.14 | 3.32 | 3.22 |
| 21:45 | 2229 | UCD Dublin vs Shamrock Rovers | 17.48 | 6.80 | 1.12 |
| 21:45 | 3555 | Everton vs Crystal Palace | 1.86 | 3.43 | 3.98 |
| 22:00 | 1669 | Chelsea vs Leicester | 1.35 | 4.88 | 7.36 |
| 22:00 | 3341 | Utrecht vs Vitesse Arnhem | 1.94 | 3.57 | 3.52 |
| 22:00 | 5043 | Aston Villa vs Burnley | 1.99 | 3.42 | 3.51 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi

Nipa


UKURASA 21



**Barca yataja sababu kumpotezea Mbappe**

**AMEULA!...**




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. bilioni 1.2, Florian Valerian Massawe, baada ya mwishoni mwa wiki kuibuka mshindi wa Jackpot ya SportPesa kwa kubashiri kwa usahihi mechi 13. Makabidhiano hayo yalifanyika katika Ofisi za SportPesa jijini Dar es Salaam jana. **Habari ukurasa wa 23. PICHA: SPORTPESA**

# DJUMA 'OUT' YANGA VS MBEYA KWANZA

●●●Ni wakati wakianza msako wa pointi 11 tu kutawazwa ubingwa, kocha asema ni kutokana na...

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI ikihitaji pointi 11 tu katika mechi zake sita zilizosalia ili kutangazwa rasmi kuwa mabingwa wapya wa Ligi Kuu Bara, Klabu ya Yanga Jumamosi itamkosa mkali wake wa pasi za mwisho, beki wa kulia, Shaban Djuma, itakapoikaribisha Mbeya Kwanza katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Yanga ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 60 baada ya mechi 24, inahitaji alama 11 tu ili kufikisha 71, ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote kati ya 16 zinazoshiriki kinyang'anyiro hicho msimu huu.

Simba iliyopo nafasi ya pili ikiwa na pointi 49 zilizotokana na michezo 23, kabla ya mechi yake ya jana ugenini dhidi ya Azam FC, kama itashinda mechi zake zote ukiwamo wa jana (kama imeshinda), itafikisha pointi 70, moja nyuma ya Yanga endapo vinara hao watavuna alama 11 katika michezo yao sita iliyobaki.

Hata hivyo, kuelekea mchezo wa Jumamosi dhidi ya Mbeya Kwanza, ambao Yanga itakuwa ikipigana kufa au kupona ili kupata ushindi na kuendelea kujenga matumaini yao ya kutwaa ubingwa huo mapema kabla ya ligi kumalizika, itamkosa Djuma ambaye atakuwa nje ya uwanja akitumikia adhabu ya kadi tatu za njano.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Kocha Msaidizi wa Klabu ya Yanga, Cedric Kaze, alisema wanaendelea kujiandaa kwa mechi hiyo lakini watamkosa Djuma.

"Tunashukuru tunaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya mchezo wetu ujao, tunamheshimu mpinzani wetu kwani msimu huu hakuna timu ya kuibeza.

"Tutaendelea na mazoezi leo jioni, kitu ambacho tunashukuru mpaka sasa hatuna majeruhi, isipokuwa tutamkosa mchezaji wetu Djuma Shaban, ambaye ana kadi tatu za njano, ila lengo letu la pointi tatu kwenye mchezo huo lipo palepale," alisema.

Djuma amekuwa msaada mkubwa katika upishi wa mbao Yanga, kwani hadi sasa ni miongoni mwa wachezaji wanne wenye pasi za mwisho ('assists') nyingi (nne), kwenye ligi hiyo ambayo ipo raundi ya 24.

Mbali na Djuma, wachezaji wengine wenye 'assists' nne hadi sasa ni Pius Buswita wa Ruvu Shooting, Tepsi Evance (Azam FC), Christian Zigah (Biashara United) na Aboubakar Ngalema wa Dodoma Jiji FC.

Aidha, Kaze alisema lengo lao ni kuendelea kushinda ili kutwaa ubingwa huo msimu huu ambao wameukosa kwa misimu minne sasa.

"Msimu huu mikakati yetu ni kuchukua ubingwa na hilo litawezekana kwa kuendelea kufanya vizuri katika michezo yetu iliyobaki," alisema.

Baada ya mechi hiyo, Yanga itasafiri kwenye jijini Mwanza tayari kwa mechi yao ijayo dhidi ya Biashara United kabla ya kubaki katika jiji hilo ikiisubiri Simba kwa mchezo wa nusu fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini, FA Cup utakaopigwa Uwanja wa CCM Kirumba Mei 28, mwaka huu.

## Mpole aanika ndoto za Ulaya



**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI akizidi kukimbiza kwenye mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu Bara, straika wa Geita Gold FC, George Mpole, amesema malengo yake ya muda mrefu ambayo anaendelea kuyapigania kila uchao ni kucheza soka la kulipwa Ulaya.

UK. 20

## Julio achekelea pointi 6 siku moja

**Na Adam Fungamwango**



KOCHA Msaidizi wa Namungo FC, Jamhuri Kihwelo 'Julio', ameonyesha kufurahishwa na timu yake kupata pointi sita kwa siku moja, wakati ikiichapa Biashara United mabao 2-1 juzi kwenye Uwanja wa Nyamagana Mwanza...

UK. 20

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >